# Mbingu Imenikirimu

# Mbingu Imenikirimu

Compiled by Unknown

Al-Islam.org

**Publisher(s):**

Al-Itrah Foundation [1]

Kitabu hiki kina eleza kwa ufupi kuhusu Imani-itikadi ya mashi'a, pia kinajibu tuhuma wanazoelekezwa wafuasi wafuasi wa Ahlul bayt a.s. yaani mashi'a. Mada zilizojadiliwa zinaeleweka na msomaji wa kiwango chochote cha elimu. Vitabu vilivyo tumiwa kutoa ushahidi (wa majibu) zinakubaliwa na Madhehebu zote na rejea zimenukuliwa kutoka vitabu sahihi vya Kisunni.

Get PDF [2] Get EPUB [3] Get MOBI [4]

# Neno la Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la "Ikramataniy Al-Samai" kilichoandikwa na Mwanachuoni mkubwa, mwanahistoria na mtafiti Mar'wan Khaliyfat.

Kitabu hiki kama kile cha "Ukweli wa Ushi'a" ni utafiti na mjadala juu ya hitilafu baina ya Shi'a na Sunni. Mwandishi ametumia njia nyepesi sana ya kumuwezesha kila msomaji wa kiwango chochote kuweza kuelewa mada zote alizozijadili katika kitabu hiki.

Katika kufanya hivyo ametumia vyanzo sahihi na vinavyokubaliwa na Madhehebu zote, ambapo rejea nyingi amezinukuu kutoka vitabu sahihi vya Kisunni.

Nia na madhumuni ya mwandshi sio kuleta malumbano, bali kufahamiana na kuleta mkuruba baina ya madhehebu hizi. Ni ukweli ulio wazi kwamba maadui wa Uislamu huzitumia sana hitilafu zetu hizo ili kutugombanisha wenyewe kwa wenyewe. Ukweli ni kwamba hitilafu hizi sio za msingi za kuweza kutugombanisha, wala haziwezi kumtoa mtu katika Uislamu. Kinachoweza kumtoa mtu katika Uislamu ni kuacha moja ya Misingi mikuu ya Uislamu, nayo ni mitatu:

- Tawhid (Upweke wa Allah)
- Nubuwwat (Utume-Adam (a.s) akiwa wa mwanzo na Muhammad (s.a.w.w) akiwa wa mwisho).
- Qiyamah (Siku ya Hukumu)

Shi'a wanamkubali Mwislamu yeyote mwenye kuikubali misingi hii kama ndugu yao katika imani. Ama Adil na Imamat, hii ni misingi ya imani ambayo hukubaliwa na shi'a tu. Lakini kama mtu haikubali misingi hii miwili ya imani, haambiwi kwamba yeye sio Mwislamu. Misingi yote hii mwandishi ameijadili katika kitabu hiki.

Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imekiona kitabu hiki ni chenye manufaa kwa Waislamu hususan wa

zama hii tuliyonayo, hivyo kama ilivyo ada yetu tumeamua tukitoe kwa lugha ya Kiswahili, kwa lengo letu lile la kuwahudumia Waislamu wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru Ndugu yetu Abdul-Karim J. Nkusui kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vile vile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni mwanga kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu katika dini.

# Dibaji

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu**

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): "Nimewaacha katika njia iliyowazi, usiku wake ni kama mchana wake hatotoka humo baada yangu isipokuwa mwenye kuangamia." (Musnad Ahmad J:4 uk:126).

"Hakika mimi nimekuachieni ambayo kama mtashikamana nayo hamtapotea kamwe baada yangu kimojawapo ni kitukufu kuliko kingine, kitabu cha Mwenyezi Mungu, kamba yenye mnyororo kutoka mbinguni hadi ardhini na kizazi changu watu wa nyumba yangu, na havitatengana hadi vinijie kwenye birika, basi angalieni namna gani mtanitafuta kwavyo."

(Sahihu Sunani Tirimidhiy-kitabul-manaqibu na Al-Albaaniy, na inayofanana na hiyo Sahihi Muslim kitabu fadhailis-Sahaba; babu mini fadhail Aliyi bin Abiy Twalib).

## Vitabu Vya Rejea

Qur’an Tukufu

Aadabu Shaafiy wamanaqibuhu- cha Ibnu Abiy Hatim Ar-Raaziy- Taasisi ya Kiislam ya usambazaji - Thagafa -Islamiyat- Misri - 1372H

Al-Ikham fiy Usuulil Ahkam - cha Ibnu Hazim Al- Andalusiy amefariki 456H chapa ya Darul -Jayli Beirut chapa ya pili 1407H

Aslu Shi’a wa Usuuliha - cha Muhamad Husein Al-Kashiful Ghit waa- amefariki 1373H

I'ilaamul-Mauqiain an Rabil alamiyna cha Muhammad bin Qayim Al Jauziyah amefariki 751H chapa ya Darul Jayli Beirut

Al-Intiqaau - cha Ibnu Abdu Barr Animriy amefariki 463H

Awailul-Maqaalati- cha Muhammad bin Muhammad Nuuman Al- Baghdadiy Al-Mufiyd amefariki 413H

Badai'us Swanaai'u- cha Al-Kasaaniy Al-Hanafiy

Al-Bidayat wanihay- cha Ibnu Kathyri Ad-Dimishiqiy, amefariki 774H chapa ya Darul-Fikri - Beirut -1402H

Tarikhu Baghdad- cha Khatibul-Baghgad amefariki 463H chapa ya Darul-Kutubil - Arabiy Beirut

Tarikhu Madinati Dimishiq - cha Ibnu As-Saakir amefariki 571H chapa ya Darul - Fikri Beirut 1416H.

Taasiysun Nadhar- cha Abu Yazid Adabusiy Al-Hanafiy - kimehakikiwa na Kusahihishwa na Mustafa Muhammad Al- Qabaaniy Ad-Dimishiq

Tadhikratul Hufaadh- cha Shamsu Diyni Adhahabiy - amefariki 748H chapa ya Darul Ihiyai turathil-arabiy - Beirut.

Tafsiru Ibnu Kathyr - cha Abul-Fidai Ibni Kathr Ad-Dimishiq - amefariki 774H chapa ya Darul Maarifat Beirut chapa ya pili 1408H

Tafsir ya Durul-Manthur - cha Jalalu Diyni As-Suyutwi amefariki 911 H chapa ya Beirut chapya kwanza ya 1403H.

Tafsiri Mafatihul Ghaib - cha Fakhru Diyni Raaziy amefariki 606 chapa ya Darul-Ihiyai Turathil-Arabiy chapa ya Beirut - chapa ya kwanza 1415H

Tafsiri Twabariy - ya Ibnu Jariyr At-Twabariy amefariki 310H chapa ya Darul - Maarifat - Beirut - chapa ya kwanza 1329.

Tafsiri Fatuhul Qadiyr - ya Muhammad bin Ali Ashaukani- amefariki 1250H - chapa ya Darul - Maarifat - Beirut.

Tafsirul- Kashaaf- ya Muhammad Jaarallah Az-Zamakhishariy- amefariki 538-Darul-Darul Maarifat - Beiruti

Talbiysul-Ibilisiy - cha Jamaalu DiyniAbul Faraj bin Jauziy amefariki 597H, kimehakikiwa na Sheikh Muhyidiyn Muhammad Bi'uyun chapa ya Darul Ibni Zaydun - Beirut - chapa ya kwan- za

Jamiu Bayaanil – ilimi wafadhlihi – chapa ya Ibnu Abd Barr An Namri amefariki 463H – kimehakikiwa na Abiy Al- Ashibaaly Azahiyriy- chapa ya Ibnul Jauziy- Saudia – chapa ya pili 1416H

Hujjatu llahil -Baalighat- cha Waliyullah Dahlawiy

Radu alaa man Akhlada ilal ardhi waankara anna Al- jithaada fiykuli 'asri faradhun cha Jalalu Diyni As-Suyitwiy amefariki 911H.

Sil silatul-Ahaadith As-Sahiha – chapa ya Muhammad Nasru Diyni Al-Albaniy – chapa ya Riyadh – 1415H

Sil silatu- Ahadith Dhaifat- cha Muhammad Nasru Diyni Al- Albaniy – chapa ya Beirut chapa ya tano 1405H

Sunanu Ibnu Maajah- ya Abu Abdillah Muhammad bin Yazid bin Maajah Al-qazuwiny amefariki 275 chapa ya Darul – Fikri Beirut

Sunan Abiy Daud ya Abu Daud As-Sajastaniy amefariki 275H chapa ya Darul – Fikri Beirut

Sunan Tirimidhiy ya Abu Isa Muhammad bin Isa bin Surat Tirmidhi amefariki 279H chapa ya Darul-Ihyai turathil Arabiy Beirut

Sunanu Darimiy -ya Abu Muhammad Abdillah bin Abdur-rahmani As-Samarqandi Adarmiy amefariki 255 chapa Darul-Fikri- Beirut

Sunanul-Kubra-ya Abubakr Ahmad bin Al- Husein bin Aali Al- Baihaqi amefariki 458H chapa ya Darul-Fikri-Beirut

Sunanu Anasaaiy-Sharhu ya Al-Haafidh Jalalu Diyni As-Suytwiy-Daru Ihiyai turathil-Arabiy-Beirut

Sharhu Nawawiy katika Sahihi Muslim-ya Muhyi Diyni Abiy Zakariya An-Nawawiy amefariki 676 H chapa ya Darul-Kutubil- ara biy-Beirut

Sahih Bukhary-ya Abu Abdallah Al-Bukhari amefariki 256 H chapa ya Aalamul-Kutubi-Beirut chapa ya pili 1406 1-1

Sahih Muslim ya Muslim bin Hajaj An-Nisabury- amefariki 261H Darul – fikri Beirut chapa ya pili 1398H

Sahih Swifat Swalati Nabiy (s.a.w.w) cha Hasan bin Ali As- Saaqaf -Darul -Imam Nawawiy – Aman Jordan chapa ya kwanza 1413H

As-Sawaiquil Muhriqat alaa Ahli rafudhi wadhalaal wazan-daqah- chapa Ibnu Hajar Al-Haitamiy amefariki 973H chapa ya Muasasatu risaalati Beirut- chapa ya kwanza 1417H

Fathul- Barr – Sharhu ya Sahih Bukhariy ya Ibnu Hajar Al- Asiqalaaniy – amefariki 852H Darul Ihiyai

Turathil- Arabiy - Beirut chapa ya pili 1402H

Fiqhu Sunna - ya Sayyid Saabiq - Darul Fatih lil'iilaamil- ara- biy - chapa ya kwanza 1418H

Kanzul-Umaal - ya Al-Mutaqiy Al-Hindiy- amefariki 975H chapa ya Muassasatu risaatat- Beirut- chapa ya tano 1405H

Majmau Zawaid na Mambaul- Fawaid- cha Abubakar Al- Haithamiy - amefariki 807H- Darul Kutubil - Arabiy- Beirut

Majumatu rasailu Al- muniyriyat cha Aswanaaniy chapa ya Darul ihiyai turathil- Arabiy- Arabiy- Beirut 1405 H

Al- Mustadrak Alaa Sahihaini cha Abu Abdillah Al- Hakim An-Nisapuri amefariki 405H Darul Fikri Beirut - 1398H

Musnad Al- Imam Ahmad bin Hanbal - amefariki 241H

Muwatwa Maalik cha Malik bin Anas amefariki 279H ihiyai turathil- arabiy Beirut

Warakibtu Safinati - cha Mar'wan Khalifat chapa ya Markazil- Ghadiyr lidiraasatil- islamiya Qum- chapa ya kwanza 1418. Na vitabu vinginevyo kati ya vitabu vya rejea.

# Utangulizi wa Chapa ya Kwanza

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye aliwatuma Mitume wake kwa ubainifu na akateremsha pamoja nao vitabu na mizani hali ya kuwa ni rehema na uongofu kwa watu. Rehema za Mwenyezi Mungu zimshukie mteule Muhammad na Ahali zake waongofu rehema ya daima isiyo na mipaka, idadi wala kikomo.

Baada ya kuchapishwa kitabu chetu "Warakibtus-Safina" watu walikipokea kwa mapokezi mazuri na wakakisifu kwa sifa nzuri, na wakushukuriwa ni Mwenyezi Mungu, baadhi yao wakanishauri kukifupisha kitabu, fikra hii inaweza ikawa sawa, kwani kitabu hicho kinazidi kurasa mia sita na sio kila mtu anaweza kukisoma au kukinunua, kwa sababu hii ndipo nikakifupisha.

Ama kitabu cha asili kinazungumzia kisa cha kuhama kwangu kutoka madhehebu kwenda madhehebu mengine, kwa ajili ya kuutafuta uislamu sahihi nalo ni jaribio la kufikia katika mfumo wa Mwenyezi Mungu ambao umefafanua uislamu kupitia njia tatu za kifikra zilizopo na ambazo zinaonekana katika medani nazo ni:-

1-Kufuata maimamu wanne wa Kiash'ariy

2-Kufuata Salafu (Salafia)

3- Kufuata Ahlul - bait (Shi'atul- imamiyah)

Na kwa kuwa utafiti huu ni muhtasari, nimelazimika kuutoa katika njia mbili ya kwanza na ya tatu, na anayetaka kusoma nadharia ya salafia ni juu yake kurejea katika kitabu chetu (Warakibtus - Safina).

Namuomba Mwenyezi Mungu anipe taufiq ya kuandika kitabu maalum juu ya salafia katika wakati mfupi ujao, na awanufaishe waislamu na utafiti huu, hakika yeye ni mbora wa kuon- goza na mbora wa kunusuru.

# Utangulizi wa Chapa ya Pili

Shukrani zote ni za Mola wa viumbe, amani na rehema za Mwenyezi Mungu zimshukie Muhammad na Ahali zake wema watoharifu.

Giza halijaacha kueneza nguvu zake za upofu ili kuzuia mwanga wa nuru tukufu ya Mwenyezi Mungu, na linajaribu kuziba kila njia wanayoifikiria wapenzi watukufu katika kuingia humo, lakini jua linatoa mwanga wake juu ya ardhi bila ya kujali mkusanyiko wa mawingu yenye giza nene, ambayo yameafikiana kuzuia nuru yake.

Hakika haki haiachi kutoa wito wake, na wengi wameshaikubali na imewafungulia milango yake ili wapate humo uongofu na maana bora ya maisha, na mchango wetu katika kuondoa vizuizi ambavyo vinafunika mbingu. Tumeona ni bora kuchapisha kitabu chetu "Warakibtus-Safina" ambacho kimechapishwa kwa jina la "Nahawul-Islaamis-Sahihi" na tumeshakirejea kwa masahihisho ya maudhui yake kwa namna ambayo tunataraji itamridhisha msomaji mtukufu.

Mar'wan Khaliyfat Iribad - Jordan

# Mwanzo wa Safari

Mbingu inaiangazia ardhi, na kuangaza njia zake zinazopitika, mwanadamu hajui lugha yake, na wakati mwingine hufanya njama bila ya kuelewa ili kuzuia mionzi yake pamoja na yote hayo halichoki, mikono yake inabaki imekunjuka ili huenda ataongoka yule atakayeikamata na kupata uongofu.

Jua linaelea angani na udanganyifu umemeza sehemu kubwa miongoni mwa nuru yake katika wakati huu, na katika moja ya njia za kijiji changu kilichojawa na ugeni, ilinijia taufiq iliyokuwa imejificha katika maneno ya rafiki yangu ambaye amekuwa rafiki yangu tangu utotoni.

Nilijadiliana naye mara nyingi ili avue itikadi yake ambayo aliichukua kutoka kwa Ahlul-Bait (a.s) na avae Usunni, ulikuwa ni wakati wa mjadala mkali kati yangu na yeye, nilitamani aingie katika madhehebu yangu. Siku zikapita nikasajiliwa katika kitivo cha Sheria na masomo ya Kiislam, ambapo waalimu wangu walikuwa hawawataji Ahlul-Bait (a.s) kwa kheri.

Pamoja na kwamba mimi nilikuwa katika madhehebu ya Shafi, isipokuwa nilianza kuathirika kwa yale waliyofundisha waalimu wangu wa kisalafia katika yanayohusu itikadi, basi nikaanza kukariri mafunzo ya itikadi ya salafia. Kadhalika yale yanayosemwa juu ya Shi'a darasani ili nianze kumuongoa rafiki yangu lakini alikuwa ananijibu kwa hoja zenye nguvu.

Na katika matembezi yetu wakati nilipokuwa namsimulia juu ya fadhila za Abubakari na Omar akanikata kauli kwa kusema - kama vile mwenye kunusurika - "huzuni ya siku ya Alhamisi!" Nikasema: "Kheri, unakusudia nini?" Akasema: "Hakika hilo ni tukio lililotokea kwa siku chache kabla ya kifo cha Mtume (s.a.w.w) ambapo Mtume (s.a.w.w) aliwaambia masahaba wake: "Njooni niwaandikie maandiko hamtapotea kamwe baada yake," Omar akasema: "Hakika Mtume amezidiwa na maumivu, au anaweweseka, kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu."

Nikamwambia: "Nyinyi mmefikia kunasibisha maneno haya kwa Al- Faruuq, ambaye hakumuasi Mtume katu?" Akasema: "Tukio hili utalikuta katika Sahihi Bukhariy na Muslim"[1]

Hapo nikakata tamaa kutokana na jibu lake, nikahisi kushindwa na nikasema haraka: "Hata kama amesema hayo bado anabaki kuwa sahaba." Namuomba Mwenyezi Mungu msamaha. Sentensi hii haikuja bure tu, bali ni ishara juu ya itikadi iliyokita mizizi katika akili zetu. Nikamuuliza: "katika kitabu gani umesoma tukio hili?" Kwa sababu mimi hata kama nitasimama msimamo wa mpingaji aliyeshindwa na kukiri, lakini nilikuwa nateketea kwa uchungu.

Akasema: "katika kitabu cha mmoja wa maulamaa wa Sunni ambaye ameingia katika madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s)." Nikaomba kitabu kutoka kwake nikaanza kukisoma upesi, baada ya kukipokea, na huzuni ya Alhamisi inazunguka katika akili yangu na nilikuwa naogopa kulikuta tukio hilo. Kikanivutia kisa cha mwandishi, nikasoma hoja za uimamu wa Ahlul-Bait (a.s) na baadhi ya masahaba mashuhuri kumhalifu Mtume (s.a.w.w) na huzuni ya Alhamisi na mwandishi anathibitisha kila tukio katika vitabu vyetu sahihi vinavyozingatiwa, nilishangaa niliposoma na nikahisi mategemeo yangu yote yameporomoka, nikajaribu kuikinaisha nafsi yangu kwamba haya matukio hayapo katika vitabu vyetu.

Na katika siku ya pili niliazimia kuhakikisha hoja hizo katika maktaba ya chuo na nikaanza na huzuni ya Alhamisi nikaikuta imethibitishwa katika Sahihi Bukhariy na Muslim kwa njia mbalimbali.

Mbele yangu kulikuwa na hiyari mbili. Ama nimuafiki Omar juu ya kauli yake kwamba Mtume

anaweweseka – Mwenyezi Mungu– apishe mbali na kwa hiyo nitaondoa tuhuma kwa Omar na ama nimtetee Mtume (s.a.w.w) na nikiri kwamba masahaba chini ya uongozi wa Omar walifanya kosa kubwa katika haki ya Mtume (s.a.w.w) hadi akawafukuza, na hapa nitaivua mbele ya rafiki yangu itikadi ambayo mara nyingi nimeikariri na kujifaharisha nayo mbele yake.

Katika siku hiyo rafiki yangu aliniuliza juu ya usahihi wa yaliyomo ndani ya kitabu, nikasema na moyo wangu unateketea kwa uchungu, "ndio ni sahihi."

Nikabaki muda mrefu nikiwa na bumbuwazi rafiki yangu akanionyesha kitabu "Liakunu ma'as-swadiqiyna" mtunzi wake ni Tijaani na kitabu chake kingine Fas'al ahla dhikri" na vinginevyo, vitabu hivyo vikafungua mbele yangu uhakika mwingi, bumbuwazi na shaka yangu ikazidi.

Nilijaribu kuzuia pumzi za bumbuwazi langu kwa kusoma majibu ya maulamaa wetu juu ya ukweli uliotajwa lakini havikunifaa bali vilinizidishi'a mwanga juu ya ukweli wa madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s) hadi ilipokamilika picha ya ukweli katika akili yangu na nikaingia katika madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s) kwa kukinaika na kwa utulivu wa moyo.

Na ndio hivi sasa na baada ya kuhitimu katika kituo cha sheria, nina yakini tosha juu ya usahihi wa ninayofuata, na nasema maneno haya na huku inanijiia katika akili yangu, namna gani niliazimia juu ya kumuongoa rafiki yangu Mshi'a na watu wake, mambo yakawa kinyume – yeye ndiye akawa, kwa taufiq ya Mwenyezi Mungu, ni sababu ya kuongoka kwangu. Sisahau neema hiyo – rehema ya Mwenyezi Mungu ambayo ilikuwa inanifuata daima, shukrani ni zako ewe Mola wangu shukrani nyingi zinazolingana na utukufu Wako mkubwa na neema Yako kubwa.

1. Rejea tukio hilo katika Sahihi Bukhary kitabu Al-maradhu watwib babu Qaulul- maridh Qumuu aniy, Sahihi Muslim kitabu ul-waswiyat babu tarkul-waasiyatu, Twabaqaatu Ibnu Saad Juz. 2. uk. 37

# Maudhui Haya ni ya Nini?

Mtume (s.a.w.w) alitupa habari kwamba umma wake utagawanyika makundi sabni na tatu, yote yataingia motoni isipokuwa moja litaingia peponi.[1] Na leo tunaona kwamba waislamu wako makundi mengi na kila moja linadai liko katika haki, na nimeona jambo hili ni muhimu sana na kwayo imesimama hatima ya waislamu, hivyo ni muhimu sana kwa kila mwislamu anayetaraji nusura siku ya Qiyama lazima ajitahidi kujua kundi hili na kulifuata.

Al-hamdulillahi mimi nimeshafanya hivyo, baada ya utafiti mkubwa, nimeshalipata kundi hili, imenithibitikia kwa dalili ya kiakili na ya kunukuu kwamba ndilo lenye kufaulu na nitathibitisha hayo katika utafiti huu.

Na ni ajabu kwamba Mwislamu anasoma Hadith hii ya kufarikiana na wala hafanyi wajibu wake wa kisheria, katika kutafuta kundi hili, kwa uhuru na kwa maudhui, ili aondoe dhima yake na akutane na Mola wake kwa moyo uliosafi.

Ni wajibu kwa Mwislamu baada ya kupita muda mrefu tangu kuja Mtume (s.a.w.w) na kutofautiana kwa madhehebu na maoni, mifarakano mingi na makundi, afuate njia ambayo anaamini kuwa inamfikisha katika kujua hukumu zilizoteremshwa kwa Muhammad (s.a.w.w) mwenye kuteremshiwa wahyi, kwa sababu Mwislamu anatakiwa kutekeleza kwa vitendo hukumu zote zilizoteremshwa katika sheria kama zilivyoteremshwa, lakini atajuaje kwamba hizi ndizo hukumu zilizoteremshwa, na ziko kama zilivyoteremshwa?
Na waislamu wametofautiana, makundi yamegawanyika, swala sio moja, ibada haziafikiani, wala vitendo katika muamalati zote haviko katika muundo mmoja.

Atafanyaje? Ni kwa njia gani atasali? Na ni muundo gani katika maoni atafuata katika ibada zake na muamalaati zake? Kama vile ndoa, talaka, mirathi, kuuza na kununua, kutekeleza adhabu kutoa fidia n.k.

Na wala haijuzu kwake kufuata baba zake na kubaki katika aliyowakuta watu wake na rafiki zake, bali ni lazima apate yakini kati yake na nafsi yake na baina yake na Mola wake, kwani hapa hakuna upendeleo, kupakana mafuta kwa mgongo wa chupa, kutofungamana na upande wowote wala kasumba.

Lazima apate yakini kuwa amefuata njia bora, ambayo anaitakidi kuwa ametimiza dhima yake, baina yake na Mwenyezi Mungu katika majukumu aliyofaradhishiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na anayoamini kuwa hakuna adhabu juu yake wala lawama kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika kufuata kwake, na kuchukua kwake hukumu kutoka kwayo, na wala haijuzu kumgusa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lawama ya mwenye kulaumu.

"***Je, mwanadamu anadhani ataachwa bure***"[2]

"***Bali mwanadamu anaijua vizuri nafsi yake***"[3]

"***Hakika huu ni ukumbusho basi anayetaka afuate njia iendayo kwa Mola wake***"[4] na [5]

1. Rejea Hadith ya kufarikiana katika Mustadrk.ak J: 1 uk: 6.1-128 na Sunan Tirimidhiy J:5 uk:26 na Musnad Ahmad J: 2 uk: 332
2. Suratul-Qiyama:36
3. Suratul- Qiyama:41
4. Suratul - Muzzammil: 19
5. Aqaidul- imamiyah Muhammad Ridhaa Mudhafar uk:63-64

# Itikadi na Athari ya Mazingira

Hakika mazingira na nyakati mara nyingi zimekuwa na athari kubwa katika kupanga fikra ya binadamu na mwelekeo wake, ambapo urithi wa kimazingira unakuwa kadiri muda unavyopita pamoja na kuzoeleka, kimaneno na kitabia unakuwa ni ukweli thabiti ambao hawezi kuuepuka; mwanadamu akitokewa na jambo linalopinga itikadi zake, athari za kifikra za jamii yake ambazo zimeshatawala katika mishipa yake zinajitokeza bila kuhisi na kusimama kidete kupinga kila anayezikhalifu, lakini Mwislamu ambaye ni mtu adhim, dini inamlazimisha kukaribisha fikra za wengine na kuzijadili kwa uhuru na kwa maudhui.

Tukiuangalia umma wa Ki-Islamu tutaukuta uko makundi mengi "kila kundi linafurahia liliyonayo"[1] kila kundi miongoni mwa makundi ya Ki-Islamu linaona fikra zake kuwa ni katika vitu ambavyo havipaswi kupingwa[2]. Na unapojadili fikra za wengine basi unaonekana utabeba mila zao na utamaduni wao, pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anawalingania waislamu wawe wazi kwa Ahlul-kitabu tukiachilia mbali kuwa wazi baina yao, amesema Mwenyezi Mungu (Sema: Enyi Ahlul-kitabu njooni katika neno la sawa baina yetu na baina yenu, tusimwabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu na wala tusimshirikishe na chochote.[3]

Kwa nini waislamu wasiwe wazi baina yao? Kwa nini watu wa dini moja wasiwe na muamala baina yao? Je, kila mmoja wetu amechagua madhehebu yake kwa fahamu na kujua? Na baada ya kusoma na kuhakiki au amejiungaje? Lazima tukubali kuwa jambo hili litakuwa gumu sana tutakapopata mambo yanayohusiana na itikadi, mila na mambo ya kurithi ambayo yameota mizizi ndani ya mishipa yetu na nafsi zimeyazoea.

Kama utamuuliza kijana aliyezaliwa katika mji wa Najaf, je, utakuwa Shi'a kama utazaliwa na wazazi wa Kisunni? Vivyo hivyo kama utamuuliza aliyezaliwa Halab, je, utakuwa Sunni kwa njia hii kama utakuwa umezaliwa katika mji wa Najaf katika familia ya kishi'a? Hapa hawatatofautiana kati yetu watu wawili kuhusu jawabu - Hapana - ambalo tutalisikia bali tunaweza kuweka jawabu mwanzo, kuwa ni katika mambo ya kawaida ambayo hakuna ikhitilafu humo.

Tanmbihi hii peke yake inatosha kutuweka wazi juu ya ukweli halisi na inatosha kutuletea mshangao wa muamala huu mgumu, na kukimbiana unaopatikana baina yetu. Kasumba zimetufikisha kiasi hicho cha hatari, hadi kasumba kwa kitu chochote tulichokizoea mazoea makubwa zaidi kuliko kuwa kwetu tayari kushikamana na hukumu ya kisheria iliyothibiti.......

Ni kipi kinanifanya katika itikadi yangu – nijisalimishe - ni madhehebu yangu niliyoyarithi kutoka kwa baba zangu na jamii yangu ndogo kuwa ndio haki pekee? Na kwamba ndio picha iliyokamilika zaidi ya dini ya Uislamu Mtukufu kiasi kwamba hailingani na madhehebu mengine katika daraja la ukamilifu? Ni nini kilichonipelekea kwenye itikadi hii? Ni Qur'an Tukufu, Sunna takatifu, akili sahihi au ni taasubu

ambayo haina mashiko?

Kwa nini nisiweze kuitakidi kuwa madhehebu mengine ni kama madhehebu yangu? Je, si nitaulizwa kesho juu ya sababu ya kufuata kwangu na itikadi yangu ya kidini?

Swali hili muhimu ndio ambalo ni wajibu niwe na msimamo madhubuti...... mbele ya ukweli huu, hakuna pa kukimbilia kwani sote tuko sawa katika majukumu, jukumu la kutafuta, kuhakiki na kisha kuchagua msimamo sahihi wakielimu usiegemee upande wowote na usivuke mipaka. Na sote tuko sawa katika hoja ya kurejea misimamo yetu kisha kuijenga upya katika misingi sahihi.[4]

1. Suratul-Mu'minoona:53
2. Nadharia hii ni yenye makosa na ameilaumu Mwenyezi Mungu katika kitabu chake kauli hii ni kama kauli ya washirikina wa kiarabu: “Hakika sisi tumewakuta baba zetu wako katika mila na sisi ni wenye kuwafuata nyendo zao” (Zukhruf. 23)
3. Surat Ali-Imraan: 64
4. Manhaju fiyl intimail - madhihabi - kitabu cha Swaibu Abdul-hamid Uk. 15-30

# Kuondoa Kikwazo

Inaonyesha kuna kikwazo mbele yetu na ni lazima tukiondoe kabla ya kuingia ndani ya maudhui kwani mtu anaweza kusema: "Hakika kutoa maoni katika maudhui kama haya, humo kuna kupinga fikra za watu wengine na viongozi wa madhehebu.

Hakika maneno haya yanahitaji msimamo, utafiti wetu huu sio mwingine isipokuwa ni utafiti wa kielimu na jaribio la kufikia ukweli halisi na wala hatukusudii kumuudhi yeyote, na hata kama utafiti wetu utakhalifu moja ya madhehebu ya Ki-Islamu au mmoja wa viongozi, hili halimaanishi kuwa na uadui nao bali lengo la hilo ni kubainisha kukosea kwao, kosa ambalo limetokana na utafiti safi wa kielimu, na humo hakuna uadui dhidi ya yeyote wala kugusa shakhisiya ya yeyote.

Na kugundua kosa ni maendeleo makubwa kwetu katika kusonga mbele kuelekea kwenye ukamilifu.

Hakika mshangao wangu unazidi kwa mtu ambaye anafumba macho yake na kuziba masikio yake hali ya kuwa anatafuta siasa ya mbuni akidhani kuwa atanusurika kutokana na hatari inayomuandama! Hakika Hadith ya 'Umma utagawanyika mafungu 73' hayaepukiki lazima tukubali hilo, na kuvua mila ambazo zimefunika akili zetu ni hatua ya awali kuelekea kwa Mwenyezi Mungu.

# Katika Zama za Mtume (s.a.w.w)

Maswahaba (r.a) walikuwa wanarejea kwa Mtume (s.a.w.w) katika mambo yanayowatokea, naye alikuwa anawajibu kulingana na sheria ya Mwenyezi Mungu, na sisi tunajua kuwa Mtume (s.a.w.w) asingebaki milele ili watu wamrejee kwa mambo ya kidini na kidunia, alifariki (s.a.w.w) baada ya kutimiza vizuri wajibu wake, na lazima awepo atakaye bainisha vizuri sheria za Mwenyezi Mungu, ubainifu ulio kamili na sahihi ambapo Mwislamu atapata matumaini kwayo na kwamba kauli yake hii ndiyo makusudio ya sheria.

Lakini huyu atakayebainisha ambaye Mwenyezi Mungu ametuandalia ni nani? Swali hilo ndilo limegawa umma katika makundi mengi. Hakika Mwenyezi Mungu hatamkubali mwanadamu isipokuwa aamini uislamu ambao aliuteremsha kwa Mtume wake (s.a.w.w). Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "anayetaka dini isiyokuwa ya Ki-Islamu hatokubaliwa nayo na kesho Akhera atakuwa miongoni mwa wenye hasara."[1]

Lakini tutapata wapi uislamu huu ambao Mwenyezi Mungu hakubali isipokuwa huo? Je, uko kwa Ash'ariy? Na madhehebu manne? Au uko kwa Shi'a Imamiya? Au uko kwa Salafia? Au uko kwa Mu'utazila? Au uko kwa Mataridiyah? Swali linaendelea vivyo hivyo hadi tufikie kundi la sabini na tatu.

Njoo tuwe pamoja, ewe msomaji mtukufu, ili tumtafute huyu mbainishaji hadi tuchukue dini yetu kutoka kwake na tujivue na dhima yetu mbele ya Mwenyezi Mungu, tutafute mfumo wa Mwenyezi Mungu ambao umeepukana na kasoro na makosa, mfumo ambao umesimama juu ya ukweli na yakini, usio na ziada, upungufu wala mabadiliko. Njoo tuangalie katika hoja za makundi mawili yafuatayo ili tuone nafasi yake katika uislamu ili tusibakie kama wale wanaosema: Hakika sisi tunadhani dhana tu na wala sisi hatuna yakini.[2]

## Ufafanuzi wa Nadharia ya Kwanza

Ni nadharia ambayo inafuatwa na Waislamu wengi hivi leo na wao wanajiita Ahlus-Sunna wal-jamaah, wao katika misingi ya dini (usuul) wanarejea kwa Abul - Hasani Al-Ash'ariy na katika ( furu'u) wanarejea kwa maimamu wanne."[3]

Abul-Hasan Al-Ash'ariy amezaliwa 270H, na inasemekana amezaliwa 260H na amefariki 324H, na inasemekana 330H, amesoma elimul-kalaam kwa Al-Jabaiy, mmoja wa masheikh wa Mu'utazilah na baada ya miaka 40 katika muutazilah na kwa athari za mijadala mingi pamoja na mwalimu wake Al-Jabaiy; akapata maoni mahsusi yaliyomfanya aache kuwa Mu'utazilah"[4] na akaanzisha madhehebu yake yenye msimamo wa kati baina ya watu wa Hadith na Mu'utazilah "wenye kufuata akili, madhehebu yake yakawa ni kutumia akili na kunukuu, madhehebu yake yalienea baada ya karne ya sita Hijiria, Ash'aria wanafuata mmoja wa maimamu wanne wa kifiqihi nao ni:-

Abu Hanifa Nu'umani bin Thabit

Maaliki bin Anasi

Muhammad bin Idrissa As-Shaafiy

Ahmad bin Hanbali

Hawa maimamu hawakuwa katika Ash'ariy; Ash'ariy amezaliwa baada yao kwa miaka mingi, Abu Hanifa alikuwa ni Marijiah, Ibnu Hanbali na Maaliki walikuwa katika Itikadi ya watu wa Hadith.

## Ufafanuzi wa Nadharia (Madhehebu) ya Pili

Nayo ni nadharia ambayo inafuatwa na Shi'a Al-Imamiya na wao wana idadi kubwa katika waislamu na wanafuatia baada ya Ash'aria kwa idadi. Shi'a wanachukua uislamu wao - itikadi na fiqihi - kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) na watu wa nyumba yake watukufu (a.s) na wala si vinginevyo, na wanaamini uimamu wa Ahlul-Bait, kifikra na kisiasa; na muda wote wa historia walikuwa wanapinga watawala jeuri, na walipata mateso mengi na kupotoshwa shakhisiya yao na watawala na maulamaa waovu kwa muda wote wa historia ya Ki-Islamu.

Ama ni lini Ushi'a ulianza, hapa kuna rai nyingi katika kuanza kwake[5], na ambayo sisi tunaamini ni kwamba wafuasi wa Ali (a.s) walianza katika uhai wa Mtume (s.a.w.w) ambao walikuwa wanamsifu na kumuenzi, kisha jina la Ushi'a likakolea zaidi baada ya hapo.

Amesema Abu Hatimu Ar-Raaziy mwenye kitabu cha Az-Ziynah: "Hakika jina la kwanza lililodhihiri katika Uislamu katika zama ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) ni Shi'a, na hii ilikuwa ni lakabu ya masahaba wanne nao ni:-

Abu Dharri
Salman
Miqidad
Ammar[6]

Ibnu Khaldun amesema: "Kundi la masahaba lilikuwa linamfuata Ali, na likaona kuwa ana haki zaidi kuliko mwingine, na alipoenguliwa na kupewa mwingine wakachukia juu ya hilo na wakamsikitikia, isipokuwa kaumu kwa kushikamana kwao na dini na kujali kwao umoja hawakuzidisha katika huo mnong'ono zaidi ya kuchukia na masikitiko.[7]

Dkt. Subhi Swalehe amesema: Kulikuwepo baina ya Masahaba hata wakati wa Mtume (s.a.w.w) na wafuasi wa mtoto wake wa kulea Ali. Kati yao ni:-

Abu Dhar Al-Ghafaar
Miqidad bin Al-Aswad

Jabir bin Abdillah
Ubay bin Kaab
Abu Tufail Omar bin Waail

Abbas bin Abdulmutalib na watoto wake wote Ammar binYaasir na Abu Ayub Al-Answariy[8]
Na katika waliosema Ushi'a ulianza wakati wa Mtume ni Ustadh Muhammad Kurd Ali katika kitabu chake cha "Khitwatu shaami."[9]

Na Muhammad Abdillah Annan katika "Jumuiyat Siriyah" na Abdillah Al-Amin katika kitabu chake "Al-firaqu wal-madhaahibul qadiymah."[10]

1. Surat Ali-imraan:85
2. Surat Al-jathiya 32
3. Yapasa kuelewa kwamba lakabu ya Ahlus-sunna wal-jamaaah ni pana zaidi Ash'ari anaingia humo Al-metaridiyah, Adhahiriyya Al-hashawiyah, na watu wa Hadith, kusema kweli lakabu hii - kwa Ash'ariah ni kwa upande wa ujirani (Ukuruba) kwa kujiita kwao lakabu hiyo
4. Alipata sababu zingine labda zilizomsababisha kufuata jambo hili hapa sio mahali pa utafiti wake
5. Baadhi yao wamesema ushi'a umeanza siku ya saqifa na inasemekana siku aliyouliwa Athumani na inasemekana umeanzishwa na Abdillahi bin Saba'a ......
6. Raudhaatul jannaat 88
7. Tarikhu Ibnu Khuldun Juz.3 uk 364
8. Anudhumul - islaamiyah, uk 96
9. Khitwatu shaam J 5 uk 251
10. Kwa ufafanuzi wa maudhui haya rejea kitabu chetu"Warakibtus Safina uk. 616 - 619

# Utaratibu Wetu Katika Utafiti

Utaratibu wetu katika utafiti huu ni kulitaka kila kundi lilete hoja yake kutoka katika kitabu na Sunna juu ya usahihi wa madai yake kwa sababu ni wajibu kwa hao watu kuuchukua Uislam wao kwao, utarat- ibu wetu ni Qur'an, anasema Mwenyezi Mungu: "Sema leteni dalili zenu kama nyinyi ni wa kweli"[1] na “ambaye mizani ya amali zake njema itakuwa nzito, Basi atakuwa na maisha mazuri."[2]

Kwa kuongezea haya tutataja matatizo muhimu katika misingi ya makundi haya mawili kama yatapatikana: "Wabashirie waja wangu ambao wanasikiliza kauli kisha wanafuata iliyo nzuri zaidi; hao ndio ambao wameongozwa na Mwenyezi Mungu na hao ndio wenye akili."[3]

1. Suratu Tawba: 199
2. Surat ul Qaari'ah: 7
3. Surat Zumar 17 na 18

# Sehemu ya Kwanza Pamoja na Ash’ariah

Kwa nini niwe Asha'riah?

Kwa nini ni wajibu nimfuate Ash'ariy na moja ya madhehebu manne? Je, kuna dalili? Je, kuna Aya? Kuna Hadith?

Tukirejea kwenye Qur'an na Sunna hatupati hata ishara ndogo juu ya jambo hili, anasema Jaadul –haqi Ali Jaadul–haqi– Sheikh wa Azhari: "Hailazimu kauli ya mwenye kusema kuwa kuna ulazima wa kumfuata mmoja wa maimamu, Abu Hanifa, Maaliki, Shaafiy na Ahmad bin Hanbali wakati hakuna dalili juu ya hilo."1

## Maimamu Kukataza Kufuatwa Kwao

Kati ya matatizo yanayotupata hapa ni kukataza kwa maimamu wanne wao wenyewe kufuatwa na katazo hili limepokelewa kwa ishara na kwa wazi na hizi ni baadhi ya kauli zao:–

### Kauli za Abu Hanifa

Si halali kwa yeyote kufuata kauli yetu maadamu hajui tumeichukua wapi.2

Shaukani amesema katika kueleza kauli hii "Na huku ni kukataa wazi kufuatwa, kwa sababu anayejua dalili basi ni mujitahidi anayetakiwa kutoa hoja, si mwenye kufuata, kwani yeye ni mwenye kufuatwa, ambaye anafuata na anakubali kauli hatakiwi kutoa hoja."3

Kauli yetu ni maoni nayo ni maoni bora tuliyoyafikia na atakaye kuja na maoni bora kuliko kauli yetu basi yatakuwa ni bora zaidi kuliko kauli hii yetu"4 na amepokea Ibnu Hazim kauli miongoni mwa kauli za Abu Hanifa juu ya kukataza kufuatwa.

3. Ilisemwa kwa Abu Hanifa, "Ewe Abu Hanifa haya unayotolea fatwa kwayo; ni ukweli ambao hauna shaka? Akasema: "Sijui, huenda ni batili ambayo hakuna shaka humo."

Zafar anasema: "Tulikuwa tunaenda kwa Abu Hanifa na yuko pamoja nasi Abu Yusuf na Muhammad bin Al–Hasan, tulikuwa tunaandika kutoka kwake, siku moja akamwambia Abu Yusufu ole wako! Usiandike kila kitu unachokisikia kutoka kwangu, kwani mimi naweza kuona rai leo, kisha nikaiacha kesho na naona rai kesho na naiacha keshokutwa. "5

### Kauli za Malik Bin Anasi

"Hakika mimi ni binadamu nakosea na kupatia angalieni katika rai yangu, kila itakapoafikiana na kitabu (Qur'an) na Sunna basi ichukueni na yoyote isiyoafikiana na kitabu na sunna iacheni."6

Ibnu Hazim akielezea maneno ya Malik anasema: "Huyu ni Malik anakataza kufuatwa, vile vile Abu Hanifa na Shafiy".[7]

Na Shaukani amesema: "Haifichikani kwako kuwa hii ni kauli kutoka kwake yaani Maliki kwa kukataza kufuatwa kwake."[8]

Malik amesema: "Sisi tunadhani dhana tu na wala hatuna yakini."[9]

Al-Qaa'naby amesema: "niliingia kwa Malik katika maradhi yake aliyofia na kumsalimia, nikamuona analia, nikasema: "Ewe Abu Abdillah kitu gani kinakuliza?"

Akaniambia: "Ewe mtoto wa Qaa'nab, kwa nini nisilie! Na nani anahaki ya kulia zaidi kuliko mimi? Natamani nipigwe mijeledi, nilikuwa na nafasi katika niliyoyatanguliza, laiti nisingetoa fatwa kwa rai yangu."[10]

Imepokewa kuwa Malik alitoa fatwa katika talaka ya Al-battah (talaka ambayo haina kurejea) kuwa ni talaka tatu, akaangalia kwa Ashihabu naye ameshaiandika akasema: "Ifute, mimi kila ninaposema kauli mnaifanya (kama) Qur'an, unajuaje huenda mimi nitaiacha kesho na nitasema kuwa ni moja."[11]

## Kauli za Shafi

1- "Ambayo nimeyasema Mtume alikwishasema kinyume na kauli yangu, basi ambayo yamesihi kutoka Hadith ya Mtume ni bora zaidi na wala msinifuate mimi."[12]

As-Sakabiy ametoa dalili kwa kauli hii ya Sharifiy juu ya kukataza kwake kufuatwa.

"Asifuatwe yeyote isipokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu."[13]

Shafi amemwambia Maziniy: "Ewe Ibrahim usinifuate katika kila ninayosema, tazama hili kwa ajili ya nafasi yako, hakika hii ni dini."[14]

"Hakika nimetunga vitabu hivi bila ya jitihada, hivyo ni lazima kupatikana humo makosa! kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema: Kama (Qur'an) ingekuwa inatoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu basi wangekuta humo makosa mengi,"[15] mtakapopata katika vitabu vyangu hivi yanayopingana na kitabu na Sunna basi nimeshayaacha hayo."[16]

## Kauli za Ahmad Bin Hanbal

Msinifuate wala msimfuate Maliki, Shafi, Auzaaiy wala Thauriy bali chukueni walipochukulia."[17]

Abu Daudi anasema: Nilimwambia Ahmad: NimfuateAwzaiy au Malik? Akasema: Usimfuate yeyote katika dini yako miongoni mwa hawa, Chukua yaliyokuja kutoka kwa Mtume."[18]

"Katika uchache wa fahamu ya mtu ni kufuata watu katika dini yake."[19]

Ilitajwa kwa Ahmad bin Hanbali kauli ya Malik na ikaachwa isiyokuwa hiyo, akasema: "Haitazamwi isipokuwa Hadith, watu wanapata fitina (mtihani) hivi wanafuata kauli ya mtu na wala hawaijali Hadith."[20]

## Kauli za Maulamaa

Amesema Sahanun - naye ni mashuhuri kati ya wanafunzi wa Malik "sijui ni rai gani hii ambayo kwayo imemwagwa damu na kwayo tupu zimehalalishwa, na kwayo zimestahiki haki."[21]

Amesema Ibnu Abdibarri Hafidhul-Magharib: "Hakika hakuna tofauti baina ya watu wa Miji katika uharibifu wa kufuata"[22] na baada ya kunukuu aya za Qur'an katika kulaumu kufuata akasema: "Na hii yote ni katika kukataza kufuata na ni utanguzi kwa ambaye ameifahamu na akaongozwa kwa uongofu wake."[23]

Amesema kadhi Al-Baqalaaniy: "Atakayefuata basi asimfuate isipokuwa aliye hai na wala haijuzu kumfuata aliyekufa."[24]

Suyutwiy amesema: "Waliotangulia na waliokuja baadaye hawakuacha kuamrisha Ijitihadi na kusisitiza juu yake na wanakataza taqlidi (kufuata), wanailaumu na wanaichukia, na ameshatunga katika kushutumu taqlidi Al-Maziny, Ibnu Hazim, Ibnu Abdibarr, Abu Shaamah, Ibnu Qayyim Al-jauziy na mwenye Al-baharul-muhiytu.[25]

Ibnu Daqiyq Al-Iyd ambaye anahesabiwa kuwa ni mujadidu wa karne ya saba Hijiriya, anaona uharamu wa taqlidi na hakuweza kusema wazi isipokuwa wakati wa kufa kwake. Amepokea Al-Adufiy kutoka kwa Sheikh wake Imam Ibnu Daqiril-Iyd kwamba alimuomba karatasi na akaandika katika maradhi yake aliyokufa na akaiweka chini ya godoro lake alipokufa wakalitoa wakakuta kuna kuharamisha taqlidi kabisa.[26]

Amesema Sheikh-Akbar Ibnu Al-Arabiy: "Taqlidi katika dini ya Mwenyezi Mungu haijuzu kwetu, sio taqlidi ya aliye hai wala maiti."[27]

Shaukani anasema: Matamshi ya maimamu wanne katika kukataza taqlidi na kutangaza rai zao na rai za wengine juu ya Nassi (Qur'an na Sunnah) haifichikani kwa anayejua miongoni mwa wafuasi wao na wengineo, kadhalika maulamaa wanne wameongoa, wasiokuwa wao kuacha taqlidi yao na wakakataza juu ya hilo. "Hakika imesihi kutoka kwao yaani maimamu wanne - kukataza taqlidi."[28]

Al-Jauziy anasema: "Jua kwamba anayeqalidi hana uhakika katika aliyoyafanyia taqlidi na katika kuqalidi kunabatilisha manufaa ya akili kwa sababu imeumbwa ili itafiti na kufikiri."[29]

Amesema Asaydu Saabiq "maimamu wanne walikuwa wanakataza kufuatwa na wamesema: Haijuzu kwa yeyote kusema kauli yetu bila ya kujua dalili yetu, na wanasema wazi kuwa madhehebu yao ni Hadith sahihi ...[30]

Saalim Al-Bahanasaawiy anasema: "Asili katika Uislamu ni Mwislam kuchukua hukumu ya kisheria

katika kitabu na Sunna, kwa sababu hakuna uma'asum kwa yeyote hadi kauli zake na vitendo vyake viwe ni sheria kutoka kwa Mwenyezi Mungu, visivyo na makosa. Na kauli za Abu Hanifa, Malik, Shafi na wengineo, sio lazima kwa dhati yake bali ni kwa kuwa kauli za hao maimamu wanne zimetegemea kitabu na Sunna."[31]

1. Durusul-husainiyah uk. 139
2. "Al-intiqau" Ibnu Abdil barr uk. 145, Majumuatu rasailil- munirah Aswanaaniy J.1 uk 28, Hujatullahil -baaligha cha Shaha Dahalawiy J. uk 158
3. Qaulul-mufiyd ya Shaukani uk. 49
4. Tarekhu Baghidad "ya Al-baghidadiy J: 3 uk 42, Hujatullahi al-baligh J:1 uk:157. Mulakhis Abu Twalib-qiyaas wa raalji wal-Istihisan wataqilid "cha Ibnu Hazim uk: 66
5. Tarekhu Baghidad "ya Al-baghidadiy J: 3 uk 42, Abu Hanifa cha Abu Zahra
6. Jaamiu bayanil- ilmi wa fadhililhi "Ibnu Abdi Barr, kimehakikiwa na Abul- Ashibaal Azahiyr J: 2, uk 775 "Maana Qaulul-imam il-matwalabiy idha swahal- hadithu fahuwa madhihabiy "Cha Taqiyu Diyni As-sabakiy" mhakiki: Ali Nayf Buqai' uk. 125
7. Al-ihkaam fiy usuulil Ah-kaam J: 6 uk 294
8. Al-qaulul- mufiyd uk: 50
9. Jamiu bayanil -ilimi wa fadhilihi J:2 uk: 33
10. Amepokea Ibnu Abdibarr - rejea Qawlul- mufiyd uk: 79, Wafayatul- Aayan: cha Ibnu Khalkaan J. 3 uk. 246
11. Al-ihkaam fiy usulil-akhaam J: 6 uk 314
12. Adabu Shaafiy wamanaqibuhu Cha Ibnu Abiy Hatim Araaziy uk 93, Maana Qaulul-imamu - Matwalabiy cha Assabakiy uk 71
13. Radu alaa man akhilada ilaal ardh waankara Al- ijitihadi fiy kuli asri faradhun cha Suyutwiy: 138
14. Hujatullaahil balighah J :1 uk: 157
15. Suratu Nisaa: 82
16. Mukhutasarul-muamal cha Abu Shaamah Shafii uk: 60
17. Rejea iliyopita uk: 61, Majumuatu rasailil-munira J: 1 uk: 27
18. Majumuatu rasailil-munira, Juz. I"ilaamul-mauqi'iyn "cha Ibnu Qayim J: 2 uk 201
19. Majumuatu rasail-munira Juz 1 uk 27 Ibnu Qayim J: 2 uk 201
20. Radu alaa man akhilada ilal ardh uk: 134
21. Alqawlul mufiyd uk. 79 lilamul mawqiin Juz. 1 uk 79
22. Rejea iliyopita uk. 48
23. Raddu alla man akhlada ilal ardhi, Alqawlul- mufiyd uk. 48
24. Ibn Hazm ameinasibisha katika Al-hkami Juz. 6 uk. 97
25. Raddun ala man akhlada uk. 42
26. Al-qawlul mufid uk. 57
27. Al-futuhaatul-makiyah, Al-babu thamin wathamanuna (mlango 88)
28. Al-qawlul-mufiyd uk 42, 48 na 66
29. Talbiysul-Ibliysi uk 124 - 125, Al - qawlul-mufiyd uk. 66
30. Fiqihi Sunnah 1: uk. 13 - 14
31. Assunnatul- mufutara alaiha uk. 194

# Tutamfuata (Tutamqalidi) Nani?

Tukiachilia mbali kauli za maimuamu wanne katika kukataza kufuatwa kwao, tukijaalia kuwa kuna dalili, tutamfuata nani? Je, tumfuate Abu Hanifa au Malik au Shafi au Ahmad? Hakika kilicho bora kimekosekana, na kuchagua kilicho bora bila ya kuwepo kilicho bora ni uharibifu kiakili na kisheria, mfano kama tutamfuata Shafi, hii si ina maana kwamba sisi tumeweka kwa wengine alama ya kuuliza? Na tatizo ni kwamba madhehebu ya Ash'ariy ya kifiqihi ni mahala pa Ikhitilafu, watu wa Hanafiy wanasema ilikuwa ni wa kihanafy, Malik wanasema alikuwa ni wa Malik na shafi kadhalika wanasema ni Shaafiy!

## Maimamu na Sunna

Hakika anayefuatilia rai za maimamu wanne anakuta kwamba humo kuna ambayo yanakhalifu sunna, mfano wa hilo ni rai yao katika talaka, inafahamika kuwa talaka tatu kwa tamko moja, Mtume ameifanya kuwa ni talaka moja.[1] Lakini Maimamu wanne wameihesabu kuwa ni talaka tatu, itajuzu vipi kwa Mwislamu kuacha kilichosihi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) na kuchukua kinyume chake?

Al-Muhaqqiq Ibnu Daqiqil-iyd amekusanya mas'ala ambayo madhehebu ya kila mmoja miongoni mwa maimamu wanne yamekhalifu Hadith sahihi mmoja mmoja na kwa pamoja katika mujaladi mkubwa[2], Al-Albaniy ametaja mas'ala 55 humo maimamu wanne na wanazuoni wamekhalifu sunna sahihi, na Ibnu Hazim amesema juu ya Hadith ambazo wamezikhalifu maimamu na mafaqihi, kama atazifuatilia mfuatiliaji basi idadi yake ingefikia maelfu."[3]

Amesema Alaithu bin Saad: Nimehesabu kwa Malik bin Anas mas'ala sabini, yote amekhalifu sunna za Mtume na humo amesema kwa rai yake."[4]

## Kutoka Katika Fiqihi ya Maimamu Wanne

Amesema Abu Hanifa: "Kama mwanaume atakuwa Misri akampa uwakala mtu mwingine aliyeko Andalusi kwamba amuolee mke basi akamuolea, na wala wasikutane aslani katika wanayo yaona watu, kisha mwanamke apate mtoto, nasaba yake itakuwa ni ya mwanamme ambaye yuko Misri."[5]

Dabusi Al-Hanafiy amesema: "Mtu akimkodisha mwanamke ili azini naye na wala si kwa ajili ya kuwa mtumishi, na akazini naye basi hakuna adhabu juu yake, kwa Abu Hanifa.

Mtu akimuoa mahrimu yake akamwingilia naye anajua au kwa kutojua hakuna adhabu juu yake, kwa sababu sura ya kuhalalisha imesha patikana nayo ni nikahu (ndoa) hata kama hakuruhusiwa, hiyo ni kauli ya Abu Hanifa....[6]
Malik - kama mtu atanuia kumtaliki (katika Fiqhi) mke na wala asitamke basi atakuwa ameachika.

Zamakhishariy mfasiri maarufu amesema: Wakiuliza madhehebu yangu siyasemi, nayaficha; kuyaficha kwake ni usalama kwangu, wakisema ni Hanafi, nitasema kwamba wanasema mimi nahalalisha pombe nacho ni kinywaji kilichoharamishwa, wakisema ni Malik nitasema wanasema, mimi nahahalisha kula mbwa na wadudu, wakisema ni Shafi nitasema kwamba wanasema mimi nahalalisha kuoa binti * na binti ni haramu, wakisema basi ni Hanbali nitasema, wanasema kwamba mimi ni mzito wa kutatua nachukiza ninasema kuwa Mwenyezi Mungu ana viungo."[7]

## Katika Itikadi ya Ash'ariah

Annawawiy amesema: "Na madhehebu ya Sunni halikadhalika ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu sio wajibu kwake kitu chochote, ametukuka Mwenyezi Mungu bali ulimwengu wote ni miliki yake dunia na akhera viko katika mamlaka yake anafanya kwavyo atakalo, kama atawaadhibu wanaotii na wema wote na akawaingiza motoni basi itakuwa ni uadilifu kutoka kwake, na kama atawaneemesha makafiri na akawaingiza peponi basi ni juu yake hilo."[8]

Hakika itikadi hii ya Ash'ariah haina dalili bali dalili ziko dhidi yake wao kwa kujengea kanuni yao – sio wajibu kwa Mwenyezi Mungu kitu chochote – wamesema kujuzu kwa Mwenyezi Mungu kuwaingiza watiifu motoni na makafiri kuwaingiza peponi, lakini kanuni hii ni mbovu kwani Mwenyezi Mungu ameshawajibisha katika nafsi yake vitu kati ya hivyo ni rehema.

Amesema Mwenyezi Mungu: "Mola wenu amefaradhisha rehema katika nafsi yake."[9] Na waliyoyasema kwamba ulimwengu ni miliki ya Mwenyezi Mungu na Dunia na Akhera viko katika mamlaka yake amefanya kwavyo anayotaka ni sahihi, lakini mambo hayafikii awaadhibu vipenzi vyake kwani Mwenyezi Mungu ameahidi pepo zinazotiririka chini yake mito katika Aya nyingi.

"Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli."[10]

"Hakika ahadi yake ni yenye kutekelezwa."[11]

Je, ni kitendo cha Mwenyezi Mungu Mtukufu?

Kadhi Al-iyji amesema katika "Al-Mawaaqifu" katika maqsadu ya saba: Taklifu kwa yasiyowezekana inajuzu kwetu.[12]

Hii ni itikadi nyingine inayopingana na Qur'an. Amesema Mwenyezi Mungu: "Mwenyezi Mungu haikalfishi nafsi isipokuwa inachokiweza,"[13] "Mwenyezi Mungu haikalfishi nafsi isipokuwa kwa kile alichokipa."[14]

1. Sahihi Muslim, kitabu Twalaaq babu twalaaq thalaath (mlango wa talaka 3)
2. Rejea "Swifatuswalati Nabiyi" cha Al-Albaniy uk. 37
3. Al-Hadith hujatu binafsihi fiy aqaidi wal-ahkaaami cha Al-Albaniy uk. 58
4. Jamiu bayanil ilimi wafadhilihi J: 2 uk 1080
5. Al-ahawalus-shakhisiyat cha Muhyidiyni Abdul-Hamid bahath ya nasaba na rejea kitabu cha Hanafi
6. Taasisu Nadhar uk:148-149 Al-qabaaring Adimishiqiy na tazama:Badaius-swanain cha kasaaniy Al-hanafiy J:4 uk:35

*Ana kusudia kwamba shaafiy anahalalisha mtu kumuoa binti yake wa zinaa

7. Tarjama ya Zamakhishariy J: 4 katika tafsiri yake ya kashafu uk. 310
8. Sahihi Muslim, sharah ya Nawawiy J: 17 uk 160
9. Suratu Al-An-aam: 54
10. Surat Luquman: 33
11. Surat Mariyam:61
12. Al-Mawaaqifu uk 330
13. Surat Baqarah: 186
14. Surat Twalaq: 7

# Kauli za Maulamaa Kwa Maimamu

Khatibu Al-Baghdad amepokea kwa Isnad kutoka kwa Wakii amesema: walikutana Sufiyan Thauriy, Shariki, Hasan bin Swaleh na Ibn Abiy Laila; wakamwita Abu Hanifa, akawajia, wakamwambia: "Unasemaje juu ya mtu aliyemuuwa baba yake? Akamuoa mama yake na akanywa pombe akiwa amekaa juu ya kichwa cha baba yake?"

Akasema: "Ni mu'umini." Ibn Abu Laila akamwambia: "Sitokubali shahada yako abadani," Sufiani Thauriy akamwambia: "sitokusemesha kamwe," na Shariki akamwambia: "kama ningekuwa na mamlaka juu yako ningekukata shingo," Hasani bin Swalehe akamwambia: "Uso wangu kwako ni haramu kutazama uso wako abadani" ..... na aliposikia kufariki kwake Sufiyani alisema: "Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amewapumzisha waislamu kwake.[1]

Naye amesema Ibnu Abdi Barr juu yake: "katika waliomshutumu na kumkosoa ni Muhammad bin Ismail Al-Bukhariy, amesema katika kitabu chake "Al-Dhuafau wal-matruukina Abu Hanifa Annuman bin Thabit Al-Kuufiy, Naimu bin Hammadi." Amesema ametusimulia Yahya bin Said na Maadh bin Maadhi; tulimsikia Sufian Thauri anasema: "Abu Hanifa alitakiwa atubu, kutokana na kukufuru kwake mara mbili, Nuaim bin Al-fazaariy amesema: "Nilikuwa na Sufiyan bin Uyainah ikaja habari ya kifo cha Abu Hanifa," akasema: "Alikuwa anavunja Uislamu tawi kwa tawi na hakuzaliwa katika Uislamu mtoto muovu kuliko yeye, haya ni ambayo ameyataja Al-Bukhariy."[2]

Kutoka kwa Walid bin Muslim anasema: Aliniambia Malik bin Anasi, "Je, Abu Hanifa anataja mji wenu?" Nikasema ndio, akasema, "haifai kuishi katika mji wenu."[3]

Na anasema Ibnu Abdil-barr juu ya Imam Malik: Ameshazungumza Ibnu Abiyt Dhiib juu ya Malik bin Anasi maneno mabaya na makali nimeona karaha kuyataja, ni mashuhuri kwake aliyasema kwa kupinga kwake kauli ya Malik katika Hadith ya "Al-bay ain bil-khiyar"; Ibrahim alikuwa anazungumza dhidi yake, na Ibrahim bin Yahya alikuwa anaomba dhidi yake, vile vile amezungumza juu ya Malik - katika aliyoyataja As-Saajiy katika kitabu chake Al-Illal - Abdul - Azizi bin Abiy Salamah na Abdurahman bin Zaid bin Aslam na Ibnu Is'haaq na Ibnu Abiy Yahya na Ibnu Abiy Zanad na wakaaibisha madhehebu

yake, na wamezungumza juu yake wasio kuwa hao kwa kuacha kwake riwaya ya Saad bin Ibrahim, na riwaya yake kutoka kwa Daud bin Al-Hasyin na Thauri bin Zaid. Na alishutumiwa Shafi na baadhi ya wafuasi wa Abu Hanifa katika rai yake kwa hasadi kwa nafasi ya Uimam wake.

Na watu walimlaumu katika kupinga kwake kupaka juu ya khofu katika safari na pasipokuwa na safari na katika maneno yake juu ya Ali na Athumani na katika fatwa yake katika kuwaingilia wanawake nyuma."4

Ama Shafi ameshazungumza juu yake Yahaya bin Muiyn - Imam wa kurekebisha na kukosoa, amesema sio mkweli;5 Amesema, Ibnu Abdil-barr : Imesihi kutoka kwa Ibnu Muiyn kwa njia nyingi kwamba alikuwa anazungumza juu ya Shafi."6

## Na Wao Ni Wafu Vile Vile

Vipi tutawafuata katika dini yetu na wamesha kufa kabla ya miaka elfu moja na mia mbili? Mas'ala yao yaliyoandikwa hayatoshi na zama zinaendelea kubadilika, kila siku kunakuja mas'ala mapya.

## Kadhalika Wametofautiana

Hakika maimamu wanne wametofautiana baina yao, kila mmoja ana fiqih mahsusi; na sisi tunafahamu kwamba hukumu ya Mwenyezi Mungu ni moja na sio mbili kwa sababu haki ni moja na sio nyingi, watu wanaweza kutoa hoja kwa Hadith: "Hitilafu katika Umma wangu ni rehema" ili watoe kisingizio cha ikhitilafu iliyodhihiri baina ya maimamu, lakini tukifaradhisha kuwepo kwake inapingana na Qur'an, vipi Mtume atahimiza Umma wake juu ya kutofautiana naye anawasomea kutoka kwa Mola wao Mtukufu; "Nashikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote na wala msitengane"7 na kauli yake "na wala msiwe kama wale ambao waliofarikiana na kutofautiana baada ya kuwajia ubanifiu8 na kauli yake, Hakika umma wenu huu ni umma mmoja."9

Hadith hii pamoja na kuenea kwake haina sanadi na kwayo anasema Al-Albaniy: "Haina asili muhadithuna wamejitahidi ili wapate sanadi, lakini hawakupata."

Na amenukuu Al-Munawiy kutoka kwa As-Sabakiy kwamba amesema: "Haifahamiki kwa Muhadithyna na sikupata sanadi sahihi wala dhaifu, Amekiri Sheikh Zakariya Al-Answaariy katika Sharh yake katika tafsiri ya Al-Baidhawiy (Q 3/92)."10

Na amesema Ibnu Hazim juu yake: "Na hii ni katika kauli mbaya kwa sababu kama Ikhitilafu ni rehma basi kuafikiana kungekuwa ni bughudha na hili ni ambalo halisemi Mwislamu, kwani hakuna isipokuwa kuafikiana au kufarikiana, na ama ni rehma au bughudha. Na amesema katika sehemu nyingine: "Ni batili uwongo."11

1. Tarikhu Baghidad J: 13 uk 374
2. Al-ilitiqaau uk. 150
3. Al-'ilalu wa maarifatu rijaali "cha Ahmad bin Hambal J: 2 uk 547 kimehakikiwa na kutolewa na Wasiyullah Abbas na

akasahihisha Sanad zake.

4. Jamiu bayanil – ilimi wafadhilihi J: 2 uk 1115
5. Jamiu bayanil – iilimi wafadhilihi J: 2 uk 1114
6. Jamiu – bayanil – iilimi wafadhilihi uk 394
7. Suratu Ali-Imran : 103
8. Suratu Ali-Imran :105
9. Suratul-Ambiyai :92
10. Silsalatul-ahaadiythi dhaiyfah J:1, uk 76 Hadith ya 57
11. Al-Ihakam fii Usuuli Ahkaam Juz. 5 uk 64

# Mzozo Kati ya Wafuasi wa Madhehebu na Kukufurishana Baadhi Yao Kwa Baadhi

Katika aina ya mzozo baina ya wafuasi wa madhehebu ni kwamba wa Hanbali walikuwa wanachoma moto misikiti ya watu wa Shafi, makhatibu Wakihanafi walikuwa wanawalaani Hanbali na Shafi juu ya mimbari na ilitokea fitina baina ya wa Hanafi na Shafi hata masoko na madrasa zilichomwa moto.[1]

Yaaqutu Al-Hamuwiy amesema amepokea kutoka kwa Is'bahan: "Uharibifu ulienea katika wakati huu na kabla yake kutokana na wingi wa fitina na ta'asubu baina ya Shafi na Hanafi na vita vilivyoendelea baina ya pande mbili kila kundi liliposhinda lilipora maduka ya kundi jingine, kuchoma moto na kuharibu."

Na amesema kutoka kwa Arayii: "Kulitokea ugomvi baina ya Hanafi na Shafi na vita vikaanza baina yao na ushindi mara zote ulikuwa kwa mashafiy hii ni pamoja na kwamba wao walikuwa ni wachache kwa idadi isipokuwa Mwenyezi Mungu aliwanusuru."[2]

Mulla Aliyul-qaariy Al-Hanafi amesema: "Imeenea kwa mahanafi kwamba Hanafi akihama kwenda madhehebu ya Shafi anaadhiriwa na ikiwa kinyume anavuliwa toka kwayo tu."[3]

Amesema Mudhafarul-tuusiy As-Shaafiy: "Kama ningekuwa na mamlaka ningechukuwa jiziya {kodi} kwa Mahanbali."[4] Na Abubakari Al-Mughaariy aliwakufurisha Mahanbali wote.[5]

Wakati ambapo Ibnu Hatim Al-Hanbali amesema: "Ambaye sio Hanbali sio Muislam."[6]

1. Al-bidayatu wanihayah J: 14, uk 76 Miriiatul-jinan J: 3 uk 343
2. Muujammul - buldan J: 1, uk 209 na J: 3 uk 117
3. Irishadu Naqaad cha As-swanaaaniy, rejea dinul-khalis J:3 uk 355
4. Miriatu-zamaan j: 8 uk 44
5. Shadharaatu dhahab J: 3 Uk: 252
6. Tadhikratul-hufadh J:3 uk 375

# Siasa na Nafasi Yake

Linaweza kujitokeza swali katika akili kama Maimamu wamekataza watu kuwafuata wao kwa nini leo tunaona waislamu wanawafuata? Jawabu ni kwamba siasa ndio sababu, serikali dhalimu zililazimisha madhehebu manne kwa watu, wakalazimishwa kufanya ibada kwa mujibu huo, na zikayapiga vita madhehebu mengine na katika hilo, anasema mwanahistoria Al-Muqaariyzi: "Uliendelea utawala wa Makadhi wanne kuanzia mwaka 566 Hijiria hadi haikubaki Miji ya Ki-Islamu, Madhehebu inayojulikana katika madhehebu ya Ki-Islaamu yasiyokuwa hayo, na maulana wao walitoa fatwa katika Miji kuwa ni wajibu kufuata madhehebu haya na kuharamisha yasiyokuwa hayo, na yameendelea kufuatwa hadi leo. Na Bibiris akatangaza wazi kufungwa kwa mlango wa Ijitihadi na amri yake inaendelea pamoja na kwamba ufalme wake umeshaondoka."... [1]

Abdul-Mutaaliy Aswaydiy amesema: "Hakika mimi naweza kuhukumu hapa kuzuia ijitihadi kumepatikana kwa njia za udhalimu na kwa wasila wa mabavu na kwa kutoa mali na hakuna shaka kwamba njia hizi kama zingetumika kwa yasiyokuwa madhehebu haya manne ambayo tunayafuata leo yangebaki na watu wengi wanaoyafuata, vile vile, na leo yangekuwa yanakubalika kwa anayeyapinga."[2]

1. Al-khutwatul Al maqaariziy J: 2 Uk: 333
2. Maydanul- ijitihadu uk: 14

# Mwisho wa Safari

Baada ya safari hii katika Madrasatul Ash'ariah tumeona kwamba hakuna dalili inayowajibisha kuyafuata, na tumeona baadhi ya matatatizo ambayo yalidhihiri humo, na hii inatupeleka katika wito wa Ushi'a ili tuone waliyonayo.

# Sehemu ya Pili Pamoja na Shi'atul-Imamiya

Je, kuna dalili?

Swali hili hili ambalo tulilielekeza katika kundi la Sunni tunalielekeza katika kundi la wafuasi wa Ahlul-Bait (a.s); Je, kuna dalili juu ya kufuata Ahlul-Bait (a.s); Je, kuna aya? Kuna dalili nyingi katika vitabu vya Sunni na zote zinatilia mkazo juu ya wajibu wa kuwafuata Ahlul-Bait (a.s) na katika kurasa zifuatazo tutataja zilizo muhimu zaidi.

## Dalili Kutoka Katika Sunna Hadith ya Thaqalayn

Kutoka kwa Zaid bin Thabit amesema: "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu: "Hakika mimi nimekuachieni makhalifa wawili baada yangu, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, watu wa nyumba yangu na hakika havitatengana hadi vitakaponijia katika birika."[1]

Na katika Sahihi Tirmidhi na Mustadrak-as-Sahihain amesema ni sahihi: "Hakika mimi nimewaachieni ambayo kama mtashikamana nayo hamtapotea baada yangu kimojawapo ni kitukufu kuliko kingine; Kitabu cha Mwenyezi Mungu kamba yenye silsila kutoka mbinguni hadi ardhini na kizazi changu, watu wa nyumba yangu, na wala havitatengana hadi vitakaponijia kwenye birika, angalieni mtanifuatiaje kwavyo?"[2]
Na imepokewa kutoka Sahihi Muslimu kutoka kwa Zaid bin Arqam amesema : "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu siku moja alipotuhutubia katika dimbwi la maji linaloitwa Khum baina ya Makkah na Madina, alimshukuru Mwenyezi Mungu, akamtukuza, akatoa waadhi, na akakumbusha kisha akasema: "Amma baada: Enyi watu hakika mimi ni binadamu nahofia anaweza kunijia mjumbe wa Mwenyezi Mungu na nikamwitikia na mimi nimewaachieni vizito viwili, cha kwanza ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, humo kuna uongofu na nuru basi chukueni, katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na shikamaneni nacho;" akahimiza juu ya Kitabu na akasistiza humo kisha akasema: "Na watu wa nyumba yangu nakukumbusheni Mwenyezi Mungu katika watu wa nyumba yangu."[3]

### Usahihi wa Hadith ya Thaqalayn

Hadith hii ni mutawatiri katika vitabu vya Sunni kabla ya vitabu vya Shi'a na wameipokea Hadith hii masahaba 35 na Tabiina19,[4] na maulamaa wengi wamesema kuwa ni sahihi. Kati ya hao ni:
At-Tabari
Al-Hakim katika Mustadrak

Al-Haithami katika majmau zawaid, Adhahabi katika Talkhisul-Mustadrak, Ibn Kathri katika tafsiri yake; As-Suyutwi katika Al-Jaamius-Swaghiry Al-Munawiy Muhammad Is'haq.[5]

Na Ibn Hajar ameshasema: "Kisha jua kwamba Hadith ya kushikamana na hayo imepokewa katika njia nyingi na imepokewa na maswahaba zaidi ya ishirini;" na akaitoa katika njia kumi na moja zinazofanana, na katika baadhi ya njia hizo amesema: "Hiyo ilikuwa katika Hijjatul-Wida'a huko Arafa; na katika njia nyingine ni kwamba ameisema Madina wakati wa maradhi yake hali chumba chake kimejaa maswahaba wake, katika njia nyingine ni kwamba alisema hayo katika bonde la Khum, na katika njia nyingine alisema alipotoka Twaifu kama ilivyotangulia na hakuna mgongano ambapo hakuna kizuizi pamoja na kuwa alikariri hayo kwao katika sehemu hizo na nyinginezo kwa umuhimu wa kushikamana na Kitabu Kitukufu na Ahlul-Bait wake watukufu.[6]

Na katika Muhadithyna wa wakati huu Sheikh Al-Albany amesema kuwa ni sahihi.[7]

Na muhadith wa Kishafii, Hasan bin Ali Assaqaf amethibitisha usahihi wa Hadith Athaqalayn na akasema: "Hadith ya Kitabu llahi wasunnatiy, ni ya uongo na haya ni maneno yake: Niliulizwa juu ya Hadith nimewaachieni vitu viwili hamtapotea baada yake; Kitabu cha Mwenyezi Mungu na …Je, Hadith sahihi ni kwa tamko la kizazi changu na watu wa nyumba yangu?

Au ni kwa tamko la Muslim la Wasunnatiy? Tunataraji ufafanuzi wa hilo katika upande wa Hadith na sanadi yake.

Jawabu: Hadith iliyithibiti ni kwa tamko la Ahlu-Bait na Riwaya ambazo kuna tamko la Sunnatiy ni batili kwa upande wa Sanad na Matini. Saqaaf baada ya kuipokea Hadith ya Thaqalayn kutoka katika Sahihi Muslimu akasema: Hili ni tamko la Muslimu pia ameipokea kwa tamko hili Adarimiy katika Sunan yake J:2 uk 431-432 kwa sanad sahihi kama vile uwazi wa jua na wengineo…

Ama tamko la Wasunnatiy sina shaka kuwa ni la uongo kwa udhaifu wa sanad yake na uzushi wake, na kutokana na mazingira ya Bani Ummaya yakawa yameathiri katika hilo.

Na hii hapa ni Sanad na Matini yake:

Ameipokea Al-Haakim katika Mustadrak J: 1 uk 93 Hadith na Sanad yake kutoka katika njia ya Ibn Abiy Ausi kutoka kwa baba yake kutoka kwa Thaurit bin Zaid Adailiy kutoka kwa Ukrima kutoka kwa Ibn Abbas na humo kuna: "Enyi watu? Hakika mimi nimekwisha acha kwenu ambayo kama mtashikamana nayo hamtapotea kamwe, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume wake ….."

Nasema katika Sanad yake kwa Abiy Uweys na baba yake, Al- Haafidh Al-Maziniy katika Tahadhiybul-Kamaal J: 3 uk 127, katika kumueleza Ibnu Abiy Uweys na nanukuu kauli ya aliyemkosoa:-

"Amesema Muawiya bin Swalehe kutoka kwa Yahya bin Muiyin: Abu Ausi na mtoto wake ni madhaifu, na kutoka kwa Yahya Ibn Muuyn vile vile; Ibn Abi Uweys na babake wanaiba hadithi, na kutoka kwa Yahya amesema: "Amechanganya, anasema uongo si chochote."

Amesema Abu Hatimu: "Mahala pake ni kweli, alikuwa msahaulifu" na Anasaaiy amesema: "Ni dhaifu," na akasema katika sehemu nyingine: "Sio mkweli."

Amesena Abu Qasimul Laalkaaiy: "An-Nasaaiy amezungumzia sana juu yake hadi inapelekea kuachwa kwake."

Abu Ahmad bin Adiy amesema: "Na Ibni Abiy Uweys, huyu amepokea kutoka kwa mjomba wake, Malik, Hadith ngeni, hamfuati yeyote juu ya hilo."

Ninasema: "Amesema Al-Hafidh bin Hajary katika utangulizi wa Fatuhul-Barr, uk. 391 chapa ya Darul Maarifa, juu ya huyu Ibni Abi Uweys, kwa ajili hii haitolewi hoja yeyote katika Hadith zake, kwa yasiyokuwa katika sahihi kutokana na alivyomponda Annasaaiy na wengineo.

Amesema Al-Hafidh Ahmad bin Swadiq katika Fathul-Alaiy uk 15 na amesema Salmma bin Shabib: Nimemsikia Ismail bin Abiy Uweys amesema: "Huenda nilikuwa nazua kwa watu wa Madina wanapohitalifiana baina yao."

Mtu ametuhumiwa kwa uzushi, na Ibn Muiyn amemtuhumu kwa uongo, na Hadith yake ambamo humo kuna tamko la "wasunnatiy" siyo moja katika Hadith za Sahihi (Bukhari na Muslim).

Amesema baba yake Abu Hatimu Arraaziy kama ilivyo katika kitabu cha mtoto wake cha Jarhu wataadilyli J:5 uk: 12 "Hadith yake inaandikwa na wala haitolewi hoja kwayo na haina nguvu na amenukuu katika kitabu hicho hicho, Ibnu Habiy Hatim kutoka kwa Ibnu Muin kwamba amesema juu yake kwamba "sio mkweli" ninasema: "Katika sanadi kuna mfano wa hayo tuliyotangulia kuyazungumzia juu yao, haisihi hadi ngamia aingie kwenye tundu ya sindano na hasa ambapo aliyokuja nayo yanapinga yaliyothibiti katika sahihi, fikiria vizuri Mwenyezi Mungu akuongoze."

Al-Hakimu amekiri juu ya udhaifu wa Hadith, na hivyo hakuisahihisha katika "Mustadrak" isipokuwa kaitolea ushahidi kwamba ni ya uongo na sanadi yake ni yenye kuanguka, hivyo Hadith ikazidi udhaifu juu ya udhaifu wake. Na tunahakiki kwamba Ibnu Abiy Uweys au baba yake, ameiba mmoja wao Hadith hiyo ya uongo ambayo tutaitaja, na akaipokea mwenyewe, na Ibnu Muin amesema mtoto ametokana na baba na kwamba wao walikuwa wanaiba Hadith.

Amepokea Al-Hakim katika J:1 uk. 93 Hadith hiyo na "nimeshapata ushahidi wake toka katika Hadith ya Abu Huraira" kisha akapokea kwa Sanadi yake katika njia ya Adhabiy, ametusimulia Swaleh bin Mussa Al-Twalhi kutoka kwa Abdul-Aziz bin Rafiy kutoka kwa Abi Salih kutoka kwa Abu Huraira, imerufaishwa; "Hakika mimi nimeacha kwenu vitu viwili hamtapotea baada yake Kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna zangu na havitatengana hadi mtakaponifikia katika birika."

Nimesema huu ni uzushi vile vile, nafupisha maneno hapa kwa mtu mmoja katika sanadi; naye ni Swaleh bin Mussa Al-Twalahiy, na haya hapa ni maneno ya maimamu wa Hadith miongoni mwa wakubwa wa wanao hifadhi, ambao wamemtuhumu humo katika Tahadhiybul-Kamaal J:13 uk. 96; Yahya bin Muiyn amesema: sio chochote, amesema Abu Hatim Araaziy, Hadith zake ni dhaifu, amepingwa sana na wa kweli, Anasaaiy amesema; Hadith yake haiandikwi, na akasema katika sehemu nyingine; Hadith yake ni yenye kuachwa.

Na katika Tahadhiybul -Tahadhiyb J: 4 uk 355 cha Hafidh Ibnu Hajar amesema Ibnu Hiban, "alikuwa amepokea kutoka kwa wakweli ambayo hayafanani na Hadith iliyothibiti hadi anashuhudia msikilizaji kwayo kwamba imetungwa, haijuzu kutolea hoja kwayo, na amesema Abu Nuini, Hadith zake ni zenye kuachwa, anapokea Hadith zinazopingana.

Nimeshasema: “Ameshahukumu juu yake Al-Haafidh katika Taqiriyb" tarjama No. 2891 kwamba yeye ni mwenye kuachwa" na Dhahabiy katika Al-Kaashif (2412) kwamba "yeye ni mzushi, na amepokea Dhahabiy katika "Al-Mizan" J:2 ,uk. 302" Hadith yake hii katika tarjama yake kwamba ni miongoni mwa uongo wake.

Na Malik alishataja Hadith hii katika "Muwatwa "(899 no. 3) bila ya sanad wala hakuna thamani ya hilo baada ya kubainisha uongo wa sanadi yake.

Ametaja Al-Haafidh bin Abdul-Barri katika Atamhiyd J: 24 uk 331 sanadi ya tatu ya Hadith ya uongo yenye kuzuliwa akasema: Ametusimulia Abdulrahmani bin Yahya amesema ametusimulia Ahmad bin Saidi, amesema ametusimulia Muhammad bin Ibrahim Ad-Daibily amesema, ametusimulia Ali bin Zaidi Al-Faradhiy amesema ametusimulia Al-Hunaini kutoka kwa Kathiri bin Abdillah bin Amru bin Aufu kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake; nasema: "Tunafupisha kwa ubovu mmoja ulio humo nao ni Kathyri bin Abdilah, huyu ni ambaye katika Sanadi yake amesema Imamu Shaafiy: "Ni mmoja wa nguzo za uongo," na Abu Daudi amesema juu yake "Alikuwa ni mmoja wa waongo."8

Amesema Ibnu Hiban: Amepokea kutoka kwa baba yake nakala ya uzushi haifai kuitaja katika vitabu wala kupokea kwake isipokuwa katika upande wa mshangao."9

Amesema Annasaaiy na Daru Qutuniy: "Hadith zake ni zenye kuachwa: "Amesema Imam Ahmad Hadith zake zinakataliwa, sio chochote," na amesema Yahya bin Muiin: "Sio chochote."

Na sema: "Alikosea Al-Hafidh bin Hajar (Mungu amrehemu) katika: Taqiriyb" alipofupisha kauli yake kwake; kwa kusema: "Ni dhaifu" kisha akasema "Amechupa mipaka aliyemtuhumu kwa uongo" Nasema: "Hapana hakuchupa mipaka bali hiyo ndio hali halisi kama unavyoona katika maneno ya maimamu juu yake.

Na hasa aliposema Adhahabi juu yake katika "Al-Kashif: "ni muongo," naye yuko hivyo na Hadith zake ni za uzushi haifai kuzifuata wala kuzitolea ushahidi bali zinatupwa, na taufiqi ni ya Mwenyezi Mungu.

Imebainika wazi kwamba Hadith (Kitabullahi wa Itratiy) Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu ndio sahihi, imethibiti katika Sahihi Muslim, na kwamba tamko la (kitabullah wassunnatiy) ni batili, sio sahihi kwa upande wa sanad. Hivyo ni juu ya makhatibu, watoa waadhi na maimamu wa misikiti kuacha tamko ambalo halikupokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) na wawatajie watu tamko sahihi lililothibiti kutoka kwake (s.a.w.w) katika Sahihi Muslim (Kitabullah wa Ahlul-Bait) au (Itratiy)."10

Pamoja na hayo kama tutaijaalia kwa mfano - kusihi Hadith ya (kitabullah wassunnaty) basi hakuna mgongano baina yake na Hadith ya Thaqalayni, na inabaki kushikamana na Ahul-Baiti (a.s) ni sababu ya msingi ya kufaulu, na aliisha unganisha Ibnu Hajar baina ya Hadith mbili akasema; "na katika riwaya; Kitabullah wassunnaty; ndio makusudio ya Hadith zilizofupishwa kwa kutaja Kitabu.

Kwa sababu Sunna zimebainisha, ikawa kutaja kitabu imetosheleza kutaja Sunna na majina ni kwamba mkazo umekuja katika kushikamana na kitabu, Sunna na maulamaa miongoni mwa Ahlul-Bait (a.s) na tumepata faida kwa mkusanyiko huo kwa kubaki mambo matatu hadi siku ya Qiyama.11
Na kama itasihi Hadith "Wassunnatiy"basi itakuwa imehukumiwa kushikamana na Ahlul-Bait (a.s) kwa sababu Hadith ya thaqalayn ni katika Sunna za Mtume (s.a.w.w)."12

1. Sunan Ibn Majah cha Abu Asim amekitoa Al-al-baniy na amesema ni sahihi uk:337 hadithi No: 754, musnad Ahmad J:5 uk:182
2. Sahihi Tirmidhiy kitabu Manaqib J: 633, uk 3788, Mustadrak j:3 uk 148
3. Kitabu Fadhailus-sahaba babu min fadhail Ali bin Abi Twalib
4. Rejea upokezi wao katika Abaqatul-anuwar na J: 1 na J: 2
5. Rejea Hadith Thalaqayn Tawaturuhu -fiqihihu cha Ali al-Hussainiy Al-Milaainiy
6. As-Swawaiqul-Muhuriwah J: 2 uk 440
7. Silsilatul-Ahaadithis - sahihi J: 2 uk 355 - 358
8. Amenukuu Saqafu, kauli ya Imamu Shafi na Abu Daudi kutoka: Tahadhibul-tahadhiyb J:8 uk 377 chapa ya Darun-Fkri na Tahadhiybul- Kamaal J: 24 uk 138
9. Tazama Al-Majruhiina J; 2 uk 221 cha Hafidh bin Hiban
10. Swahihi swifatus-swalati Nabiyi uk 289 - 294 na toleo la Saqaf limejibu kila aliyejaribu kuisahihisha Hadith mfano: Dkt. Ali Saalusi na wengineo
11. Asawaiqul-Muhuriqat J: 2 uk 439
12. Hakika vitabu vya kisuni ambavyo vimetaja Hadith ya thaqalayn vinakaribia mia mbili kati ya hivyo ni:- Musnad bin Hanbali J: 5 uk 182. Twabaqaat Ibnu Saad J: 2 uk 192, Al- Muujamu swaaghiru cha Twabarany uk 73, Asunanul-Kubura ya Al-Baihaqiy J:10 uk :113 KanzulUmal J: 1uk:322 na ameisahihisha Al-Albaniy katika sehemu nyingi kati ya hizo ni Silsilat hadith Sahihi J:4 uk:355 Sunan Tirimidhiy na Jamius-Swaghir

# Hoja ya Hadith

Hadith ya thaqalayni iko wazi katika wajibu wa kushikamana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na Ahlul-Bait (a.s) kwa pamoja, kusalimika kutokana na upotovu haukupatikana isipokuwa kwa kushikamana navyo kwa pamoja kwa kauli yake (s.a.w.w) "kama mkishikamana navyo" na wala hakusema na kimojawapo, na katika yafuatayo ni maneno ya baadhi ya wajuzi wa Ahlus-sunna ambao wanatilia mkazo tuliyoyasema:

Amesema Sheikh Abdul-Rahman Anakishibandiy baada ya kuwataja Ahlul-Bait "vipi isiwe hivyo na wao ndio nyota za dini, msingi wa sheria zetu, nguzo za masahaba wetu, kwao umedhihiri uislamu na kuenea na kwao umekita mizizi na kumea, kisha imesihi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) amesema: "Hakika mimi nimewaachieni" ....[1]

Na amesema Aliyul-Qaariy katika "Al-Murqaatu" kuhusu Hadith hii. Na makusudio ya kuchukua kwao ni kushikamana na mapenzi yao na kuhifadhi heshima yao, kuyafanyia kazi waliyoyapokea na kutegemea kauli zao."

Nasema: "Ni dhahiri kwamba Ahlul-Bait aghalabu wanamjua zaidi mwenye nyumba na hali zake, hivyo makusudio ni wenye elimu miongoni mwao wanaofahamu mwenendo wake, wenye kusimama katika njia yake, wenye kujua hukumu zake na hekima yake kwa haya inafaa kuwa wanalingana na kitabu cha Mwenyezi Mungu mtukufu kama alivyosema: "Na anawafundisha Kitabu na hekima."[2]

Na amesema Atafatazariy katika Sharhul-maqaaswid: "Je, huoni kwamba Mtume (s.a.w.w) amewaunganisha na Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kushikamana navyo ni kunusurika na upotovu na hakuna maana ya kushikamana na kitabu isipokuwa kuchukua yaliyomo humo miongoni mwa elimu na uongofu vivyo hivyo katika Itrah.3 (kizazi cha Mtume)."

Amesema Al-Munawiy: "Kama mtashikamana na maamrisho ya Kitabu chake na mkakatazika na makatazo Yake na mkaongoka kwa uongofu wa kizazi changu, Na mkafuata mwenendo wao mtaongoka na hamtapotea kamwe."4

1. Al-'Iqidul-Wahiyd " uk:78
2. Rejea Hadith thaqalayni - Tawatur-fiqihu "na makala ambayo ilichapishwa na Darul-taqiryb-misri juu ya Hadith ya thaqalayni
3. Rejea Hadith thaqalayni - Tawatur-fiqihu "na makala ambayo ilichapishwa na Darul-taqiryb-misri juu ya Hadith ya thaqalayni
4. Faidhul – qadiriy J:3 uk:14

# Hadith ya Safina (Jahazi)

Amesema Mtume (s.a.w.w) "mfano wa Ahlul-Bait wangu kwenu ni kama mfano wa Safina ya Nuhu, atakayeipanda ataokoka na atakayeiacha ataangamia.
Wameipokea Hadith hii masahaba nane, na wafuatao wamesema ni sahihi:-Al-Haakim katika Mustadrak J: 3 uk 151.

As-Suyutuy katika Nihayatul-Afadhali fiy Manaaqibil-Aali.1

Atwaybiy katika Sharhul-Mishkaati.2 Ibnu Hajar Ashafi ambapo amesema: "Imekuja kwa njia nyingi baadhi zimezipa nguvu baadhi yake.3

Na ameisha sahihisha Hadith hii Muhammad bin Yusuf Al-Malik maarufu kwa Al- Kafi ambapo alisema baada ya maneno yake na inakuonyesha juu ya Hadith hiyo mashuhuri ambayo ni mutafaqun alaihi juu ya kunukuliwa kwake. Mfano wa watu wa nyumba yangu ni kama mfano wa Safina ya Nuhu atakayeipanda ameokoka na atakayeiacha atagharikі.4

Na Hadith imepokelewa na maulamaa zaidi ya mia moja na hamsini miongoni mwa maulamaa wa Sunni, na wameichukulia kuwa ni katika Hadith za kawaida.5

1. Iko kwenye uchapishaji
2. Rejea khulaswatul abaqaatil anuwaar cha Al-HuseinAl milaaniy uk:43
3. Swaiqul-muhuriqah J: 2 uk 445
4. Rejea Khulaswatul-abaqaatil- anwar uk 247
5. Mfano: Mustadrak J: 3 uk: 151, Al -Muujamul -kabir, Tabrani uk:130, Muujamus swaghir Tabrani, uk :78, Majmau Za

Waid cha Haitham J: 9 uk : 168, Jamius swaghir Suyuti , Uyunl akhbar Ibn Qutayba J :1 uk : 211

# Hoja ya Hadith

Hoja ya Hadith iko wazi kabisa kwamba nusra ni kupanda safina ya Ahlul-Bait, na maana ya kupanda Safina yao ni kuwafuata wao, kuwaiga, kuwasikiliza na kuwatii, amesema Ibnu Hajar Ashafi: "Kufananishwa kwao na safina kama ilivyotangulia ni kwamba atakaye wapenda, akawatukuza kwa kushukuru neema waliyonayo na akachukua uongofu wa Maulamaa wao ameokoka kutokana na giza la ikhitilalifu na atakayeacha hayo ataangamia katika Bahari ya kukufuru neema na ataangamia katika dimbwi la upotovu.[1]

## Hadith

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): "Mimi ni Mji wa elimu na Ali ni mlango wake anayetaka elimu basi auendee mlango.[2]

Amesema Mtume (s.a.w.w): "Nyota ni tumaini la watu wa ardh[3]ini kutokana na kughariki na Ahlul-Bait ni tumaini kwa umma wangu kutokana na ikhitilafu, kama kabila katika Waarabu litawakhalifu basi watakhitalafiana na watakuwa katika kundi la Ibilisi.

Amesema Mtume (s.a.w.w); "Ali yuko pamoja na Qur'an na Qur'an iko pamoja naye havitatengana hadi vitakaponijia kwenye birika."[4]

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): "Ali yuko pamoja na haki, na haki iko pamoja na Ali yazunguuka naye popote anapozunguka."[5]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alimwambia Ali (a.s): "Wewe utaubainishia Umma wangu ambayo humo wamekhitilafiana baada yangu."[6]

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): "Anayependa kuishi maisha yangu na kufa kama nitakavyokufa na kuishi katika pepo aliyoipanda miti Mola wangu, basi ampende Ali na awafuate Maimamu katika kizazi chake baada yake, hakika wao ni kizazi changu, wameumbwa kutokana na udongo wangu, wameruzukiwa fahamu yangu na elimu yangu, maangamizo kwa wanaokadhibisha fadhila zao katika Umma wangu, wenye kukata kwao udugu wangu Mwenyezi Mungu asiwape shifaa yangu."[7]

## Dalili Kutoka Katika Qur'an

Ilipoteremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hakika wale walioamini na wakafanya vitendo vyema hao ndio viumbe bora."[8]

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w): "Ewe Ali! hao ni wewe na wafuasi wako[9] na akaongezea katika riwaya: "Hakika wao ndio wenye kufaulu siku ya Qiyama."

Amekwisha tuamrisha Mwenyezi Mungu kushikamana na Ahlul-Bait (a.s) katika kauli yake. "Na shikamaneni nyote na kamba ya Mwenyezi Mungu na wala msifarikiane."[10]

Makusudio ya kamba katika Aya hii ni vizito viwili (Kitabu na Ahlul-Bait) Hadith ya thaqalayn ni dalili bora juu ya tunayoyasema, na Hadith zimefasiri kamba ya Mwenyezi Mungu kuwa ni Ahlul-Bait (a.s)."[11]

Ametuamrisha Mwenyezi Mungu kuwauliza wenye kujua kwa kusema, "Waulizeni wanaojua kama nyinyi hamjui" "[12]
Na wanaojua tulioamriwa kuwauliza ni wao Ahlul-Bait kama ilivyo katika riwaya."[13]

Na ametuamrisha Mwenyezi Mungu kuwa pamoja nao katika kauli yake.

"Enyi mlioamini muogopeni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli."[14]

Amesema Sibtu Ibnul-Jauziy: Wamesema maulamaa wa sira: Maana yake kuweni pamoja na Ali na Ahlul-Baiti wake. Ibnu Abbasi amesema: "Ali ni Bwana wa wakweli."[15]

Na wao ni ambao ametuamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwatii katika kauli yake.
Mtii Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka miongoni mwenu"[16] wenye mamlaka ni Ahlul-Bait (a.s)."[17]

Na wao ndio iliteremka kwao ayatu Tatwihir ambapo Mwenyezi Mungu amewakinga kutokana na uchafu na akawatakasa kabisa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:
"Hapana si jingine, Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea (kuwakinga na) uchafu Ahlul-Bait na kukutakaseni kabisa."[18] Aya hii imeshuka kwa Ali, Fatima, Hasan na Husein (a.s)."[19]

Na Ahlul-Bait ni ambao alitoka nao Mtume wa Mwenyezi Mungu kufanya mubahila na manaswara aliposema Mwenyezi Mungu. 'Atakayekujadili kwa hilo baada ya kukujia elimu, basi sema: "Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, wanawake wetu na wanawake wenu, sisi na nyinyi kisha tuombe na tujaalie laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo."[20]

Wafasiri wamekubaliana kuwa Aya hii imeshuka kwa As-habul Kisai, Hasan na Husein walikuwa ni katika watoto wa Mtume (s.a.w.w) na Fatima Zahraa (badala) ya wanawake wote na Ali (a.s) ni katika nafsi yake."[21]
Na wao ndio ambao Mwenyezi Mungu amefanya mapenzi yao ni wajibu kwa kila mwislamu. Amesema

Mwenyezi Mungu: "Sema sikuombeni malipo juu yake isipokuwa kuwapenda jamaa zangu wa karibu.."22 Na makusudio ya jamaa wa karibu ni Aswihabul-kisai. Ali, Fatima, Hasan
na Husein."23

Na wao ni ambao Mwenyezi Mungu amefaradhisha kuwaswalia. Amesema Mwenyezi Mungu: "Hakika Mwenyezi Mungu na malaika wake wanamswalia Mtume, enyi mlioamini mtakieni rehma na msalimieni24 Na makusudio ya kumtakia rehma Mtume (s.a.w.w) hapa ni yeye na Ahlul-Bait wake kwa pamoja kama alivyoeleza wazi katika riwaya hii......25

1. Sawaiqul Muhriqa Juz. 2. uk. 446-447
2. Wamesema hadith hii ni sahihi maulamaa wakubwa wa Ahlus-sunna wal- jamaah kama vile Yahya bin Muiyn, Twabariy katika Tahadhiybul- athaar, Al-Haakim katika Mustadrak na Al-Hafidh Al-Ashiariy Muhammad bin Swadiq ametunga kitabu akathibitisha humo usahihi wa Hadith hii akakiita "Fatuhul- mulkil-aliyi biswihati Hadith babu madiynatil-ilmi Aliyi" na rejea Al-Mustadrak J : 3 uk. 126 na 127, Usudul-Ghabah J: 4 uk. 22, Tadhikratul-Khawasi uk. 47 na 48
3. Mustadrak J:3 uk 149 amesema Hadith hii sanadi yake ni sahihi na hawa- jaitoa,Swawaiqul-Muhariqah J: 2 uk. 445 na amesema ni sahihi, Majimau zawaid J: 9 uk 147
4. Al-Mustadrak, J: 3 uk. 124 amesema Hadith hii ni sahihi katika sanad, Tabarany katika Al-Auswat, Swawaiqul Muhuqah J.2 uk. 361
5. Tarikhu Baghidad J: 14 uk 321, Muntakhabul-kanzu J: 5 uk 30 narejea Sunan Tirimidhiy J: 5 uk. 633, Mustadrak J: 3 uk. 124, Majimau zawaid J: 7 uk. 25
6. Mustadrak J: 3 uk 122 na amesema ni sahihi kwa masharti ya Bukhariy na Muslim, Kanzul-ummal J:6, uk 156 Muntakhabul-kanzu J: 5 uk 33 Tarekhu Dimishiq J: 2 uk 488 Kunuzul-haqaiq ya Munawiy uk 188
7. Huliyatul-Aauliyai J: 1 uk 86, Majmau zawaid Juz. 9, uk 108 Tarekh Dimishiq J: 2 uk 95, na rejea Kanzul-Ummal J: 12 uk 104 Hadith No.2625 Muntakhab
8. Suratu Bayina:7
9. Hadithi hii inapatikana takriban katika vitabu ishirini kati ya hivyo ni Shawahidu tanzil cha Shaukaaniy Al-Hanafiy J:2 uk 356-466, Durul- manthur J:6 uk 379, Tafsiri Twabariy J:3 uk 146, Fatuhul-qadir ya Shaukaniy J: 5 uk 477, Ruhul maaniy ya Al-Alusiy J. 30 uk 207 Aswawaiqul mu huriqah uk. 96
10. Suratul -Ali-Imran: 103
11. Rejea Ruhul maaniy J: 4 uk 16, Aswaawaqil-Muhuriqah uk 444, Shawahidu tanzil J: 1 uk 30, 177 - 180, Al-Itihaaf bihubil-ashiraaf" ya Shibrawiy Ashaafiy uk. 76
12. Suratu Nahl: 43
13. Tafsiri Twabariy J: 14 uk: 75, Tafsir Ibnu Kathiyr J:2 uk : 591, Tafsir Qurtubiy J 11 uk : 272, Ruhul Maaniy J: 14 uk. 41, Tafsir Thaalabiy
14. Suratu Tawba 119
15. Tadhikratul-khawas uk 10 na rejea Durul-manthur J: 3 uk 290 Fatuhul qadiri J: 2 uk 295 Ruhul-maaniy J: 11 uk 41 na tafsiri Thaalabiy
16. Suratun Nisaa: 59
17. Shawahidu tanzil J:1, k: 148 Hadith No. 202 - 204. Tafsiri Raaziy J: 4 uk 113, Tafsiri Baharul-Muhuyt ya Abu Hayaan Al -Andalusiy J: 3, uk 278, Tafsiru Nisaburiy katika Sharhu ya Tafsiru Twabary J: 5 uk 79
18. Suratul - Ahzaab 33
19. Sahihi Muslim kitabu Fadhalis - Swahaba babu Fadhailul-, Ahlul- Baiti Nabiyi, sahihi Tirimidhiy J: 5 uk 663, Musnad Ahmad J: 1 uk 330, Al-Mustadrak sahi- haini J: 3 uk. 133,146,147 na 158
20. Suratul Ali- Imran: 61
21. Sahihi Muslim kitabu Fadhail s-swahaba babu min Fadhaili Ali bin Abiy Twalib, Sahihi Tirimidhiy J: 5 uk 638, Mustadrak J: 3 uk 150
22. Suratus-Shuraa: 23
23. Tafsiri Twabariy J: 25 uk. 16, Tafsiri Ibnu Kathiri J: 4 uk. 112, Tafsiri Zamakhishary J: 3 uk. 467,

Tafsiri Qurtubiy J: 16 uk 22, Al-Mustadrak J: 3 uk 172

24. Suratl-Ahzaab: 56

25. Sahihul-Bukhariy kitabu Tafsiri babu Qauluhu: inna-llaaha wamalaikatahu Yuswaalunna alaa Nabiy, Sahihi Muslim kitabu Swalaat alaa Nabiy baada Tashahud, Tirimidhiy J: 2 uk. 353

# Hoja za Pande Mbili Katika Mizani

Imethibitika kwamba hakuna dalili ya kufuata madhehebu manne na wengine katika wanaojiita Ahlus-sunna juu ya usahihi wa manhaji yao, sio katika Qur'an wala katika Sunna. Ama wafuasi wa Ahlul-Bait (a.s) wanayo hazina kubwa kati ya dalili za Qur'an na Sunna juu ya wajibu wa kuwafuata wao, kama tutaweka hoja za Shi'a katika mizani na tukaweka hoja za Ash'ariah (ambazo hazipo) katika upande mwingine wa mizani basi upande wa hoja za Shi'a ungekuwa ni mzito kwa Hadith ya Thaqalayni (vizito viwili) peke yake.

Na kwa hiyo tunaona kwamba ni wajibu kuwafuata Ahlul-Bait na kuchukua kutoka kwao, na wajibu huu ni kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake (s.a.w.w) katika wajibu wa kuwafuata wao, nao ndio sababu ya pekee ya kufaulu siku ya Qiyama.

# Kisimamo Pamoja na Salafia

Salafia wanakhalifu kundi la Sunnatu wal-Jamaah katika kuchukua mafunzo ya Ki-Islamu, wakati ambapo Sunni wote wamefuata maimamu wanne na wanafanya ibada kulingana na fatwa zao, salafia wanawachukulia mabwana hawa ni kama maulamaa wengine wa waislamu, na wala uislam haujafungamanishwa kwao tu, bali kufahamu uislamu sahihi ni kurejea kwenye kitabu na Sunna kwa kunukuliwa na sahaba yeyote. Na aliyekuja baada yao.

Sisi tuna-afikiana nao katika kutegemea Kitabu na Sunna kama misingi miwili ya Ki-Islamu lakini je, inawezekana kuchukua Sunna kutoka kwa sahaba yeyote, vyovyote itakavyokuwa sira yake bila yakuiangalia hali yake kama ilivyo manhaji ya salafia? Au ni wajibu tumwingize katika kanuni ya kukosoa na kurekebisha na kusoma maisha yake, na kama utathibiti msimamo wake na umadhubuti wake katika kunukuu, ndio inachukuliwa kutoka kwake? Amepokea Bukhariy kutoka kwa Abu Wail; amesema Mtume (s.a.w.w): "Mimi nitawatangulia kwenye birika, wataletwa kwangu wanaume miongoni mwenu hadi nitakapotaka kuwapa maji watazuiliwa dhidi yangu; Nitasema: Ee mola masahaba wangu, nitaambiwa: "Hujui waliyoyazusha baada yako."[1]

Na katika riwaya nyingine: "Watanijia watu nawajua na wananijua, kisha kutawekwa kizuizi baina yangu na wao.[2]

Na kutoka kwa Abu Huraira, hakika yeye alikuwa amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) amesema: "Watanijia siku ya Qiyama kundi kati ya masahaba wangu watazuiliwa kufikia birika, nitasema: Ee Mola wangu masahaba wangu. Itasemwa: "Hakika wewe hujui waliyoyazua baada yako, hakika wao waliritadi na kurudi nyuma.[3]

Hadith hizi zinaeleza wazi kuingia masahaba motoni na tatizo hilo liliwapata salafia, hivyo wakafasiri kuwa waliokusudiwa katika Hadith ni wanafiki na walioritadi, na tafsiri hii sio sahihi.

Riwaya inabainisha sababu ya hawa kuingia motoni nayo ni kuritadi na kuzua,...na mnafiki haritadi kwa sababu yeye hakusilimu asilani na historia haikututajia chochote juu ya uzushi wa wanafiki.[4]

Tafsiri ya kuwa ni walioritadi inapingwa kwa sababu sehemu kubwa kati yao walioritadi katika uhai wa Mtume (s.a.w.w) vipi atasema kuingia kwao motoni? Na wala hawajazua kitu katika dini bali waliritadi tu na si vinginevyo, kuna riwaya inayosema: "Baada ya maswahaba kuingizwa motoni Mtume atasema: 'Sioni akiwaacha isipokuwa kama mfano wa ngamia wasio na mchungaji."[5]

Ibnu-Hajary ameseama: Na 'hamalu' kwa fataha mbili: Ni ngamia asiye na mchungaji na maana yake ni kwamba "Hataingia katika birika miongoni mwao isipokuwa wachache kwa sababu ngamia asiyekuwa na mchungaji katika ngamia ni wachache ukilinganisha na wengine."[6]

Na imekuja katika kamusi "Lisanul-Arabi na Nihayatu ya Ibnu Athiri" yaani watakaofaulu kati yao ni wachache kwa maana ya uchache wa ngamia wenye kupotea.[7]

Kwa kuongezea haya hakika kuna riwaya kutoka kwa maswahaba walio karibu na Mtume walikiri wenyewe kuzua na kubadilisha baada ya Mtume (s.a.w.w), nazo zinafasiri Hadith zilizotangulia kiasi kwamba hakubaki kwa salafia taawili yoyote au kisingizio katika Hadith ya birika (hodhi).

Amepokea Bukhari kwa sanadi yake kutoka kwa Alau bin Abdi Musayabu, kutoka kwa baba yake amesema: "Nilikutana na Baraa bin Aazib akasema: "Umefaulu; ulikuwa sahaba wa Mtume na ukambayi chini ya mti." Akasema: "Ewe mtoto wa ndugu yangu hakika wewe hujui ambayo tumeyazua baada yake."[8]

Anasi bin Malik amesema: "Sijui kitu kati ya yaliyokuwa katika wakati wa Mtume (s.a.w.w) isipokuwa machache;" akaulizwa na sala? Akasema: "Si mmepoteza humo mliyoyapoteza."[9]

Abu Dardai amebainisha balaa ya msiba na kubadilika hali ya watu waliyokuwa nayo katika zama za Mtume (s.a.w.w) Bukhary ameitoa amesema: Nilimsikia Salim anasema: Na nimemsikia Ummu Dardai amesema: "Aliingia kwangu Abu Dardai naye ni mwenye kukasirika nikasema: kipi kimekukasirisha?" Akasema: "Wallahi sijui chochote katika umma wa Muhammad isipokuwa wote wanasali."[10]

Mtume (s.a.w.w) alishabainisha hali ya maswahaba baada yake kwa sura iliyo wazi kutoka kwa Abdillahi bin Amr bin Aasi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kwamba yeye amesema. "Zitakapofunguliwa kwenu hazina za Fursi na Roma nyinyi mtakuwa ni kaumu gani?" Abdu Rahmani bin Auf akasema: "Tutasema kama alivyotuamrisha Mwenyezi Mungu na Mtume wa Mwenyezi Mungu:" Mtume akasema: "au yasiyo kuwa hayo?"

"Mtashindana! kisha mtashindana! Kisha mtafanyiana njama, kisha mtachukiana au mfano wa hayo kisha mtawaendea masikini miongoni mwa muhajirina na watawakandamiza baadhi yao."11

Na katika Hadith ya Amri bin Auf, aliwasili Abu Ubaida na mali kutoka Baharaini, Answar wakapata habari ya kuwasili kwa Abu-Ubaida, wakahudhuria sala ya Alfajiri pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) Mtume aliposali akaondoka, wakamwashiria Mtume wa Mwenyezi Mungu, akatabasamu alipowaona akasema: "Nadhani mmepata habari kuwa Abu Ubaida amekuja na chochote kutoka Baharaini, wakasema: "Ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu." Akasema; "Furahini na pendeni yanayokufurahisheni, wallahi siwaogopei ufakiri, lakini naogopa kwenu Dunia kuwanyookea kama ilivyowanyookea waliokuwa kabla yenu, mkaishindania kama walivyoishindania basi ikawaangamiza kama ilivyowaangamiza.12

Mtume (s.a.w.w) ametilia mkazo katika Hadith nyingine akiweka wazi humo kwamba Maswahaba zake watawafuata waliokuwa kabla yao, amesema (s.a.w.w): "Mtafuata nyendo za waliokuwa kabla yenu shibri kwa Shibri, dhiraa kwa dhiraa hata kama wataingia katika shimo la kenge mtawafuata."

Tukasema "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni mayahudi na manaswara? Akasema: "Ni nani basi?"13

Imetubainikia kwamba haiwezekani kwa Mwislamu kupata matumaini katika kuchukua kutoka kwa swahaba yeyote kama ilivyo manhaji ya salafia, tuna-afikiana nao katika Kitabu na Sunna, lakini watakaozifafanua kwa watu ni maimamu wa Ahlul-Bait kulingana na dalili zilizothibiti.

1. Sahihi Bukhariy kitabul-fitani babu maaja fiy qaulilahi talaa wataqUu- fitina laa twisibanna aladhiyna dhalamuu min khum khaswa
2. Sahihi Bukhariy kitabul-fitani babu maaja fiy qaulilahi talaa wataqUu- fitina laa twisibanna aladhiyna dhalamuu mii khum khaswa na sahihi muslimu kitabu fadhail babu ithibati haudhi nabiyinaa (s.a.w.w)
3. Sahihi Bukhariy kitabu riqaqi babu fiyl-haudhi
4. Haitaji chochote katika harakati zao dhidi ya uislamu na waislamu, je: Abubakar alikuwa mwerevu zaidi kuliko Mtume (s.a.w.w)? Hivyo akawavutia kati- ka uislamu na nyoyo zao zikawa safi au wao waliridhia hali ya kisiasa iliyokuwepo wakati huo na ikawastaajabishwa hivyo wakasimamisha njama zao walizokuwa wakimfanyia Mtume (s.a.w.w) na Qurani ikazifichua? Inanibainikia kuwa nukta hii ni muhimu sana kuifikiria na kuifuatilia
5. Sahihi Bukhariy kitabu riqaqi fiy haudhi
6. Fatuhul Bar J: 11 uk. 401
7. Lisanul Arabi-J:15 uk. 135, Nihayatu fiy ghariybil Hadath J:5 uk. 274
8. Sahihi Bukhariy kitabul- Maghaaziy babu ghazuwatil -hudaibiyah
9. Sahihi Bukhariy kitabu Mawaaqiti Swalati babu tadhiyi'i swalati
10. Sahihi Bukhary J:2. uk 159
11. Sunan Ibni Maajah kitabu Ifitan babu fitnatul -maali

12. Sunan Ibni Maajah kitabu Ifitan babu fitnatul -maali, Sahihi Bukhari kitabu maghazi J.5 199
13. Tumeshataja baadhi ya matatizo ya salafia katika kitabu "Warakibtu Safinah"

# Baadhi ya Maulamaa wa Ahlus-Sunna Kujiunga na Madhehebu ya Ahlul - Bait (a.s)

Kuenea kwa vitabu katika siku za hivi karibuni na kuanza kwa mijadala baina ya Waislamu jambo hili limesaidia kuweka wazi ukweli huu - haki ya kufuatwa madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s) kwa wengi miongoni mwa maulamaa wa Sunna au wataalamu wao, kwa ajili hiyo jopo la hawa maulamaa wamejiunga na madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s) na wametunga vitabu vilivyojaa dalili zilizo wazi, na haya ni majina ya baadhi yao:

Sheikh Muhammad Maraiy Al-Antwakiy ana kitabu Limadha ikhtartu madhihabash-Shi'ati madhihabi Ahlul-bait (a.s)

Sheikh Muhammad Amin Al- antwakiy ana kitabu Fiy twariqatiy ilaa tashayyui

Dkt. Muhammad Al-Tijaaniy as-Sammawiy Al-Tunisiy ana vitabu vingi kati ya hivyo ni: Thumma ihtadaitu

Al-Ustadh Swaib Abdul Hamid, ana vitabu vingi kati ya hivyo ni: Ibnu Taimiyah, hayatuhu, aqaiduhu, mauqifuhu min-Shi'ati Ahlul-Bait (a.s)

Wakili Ahmad Husein Yaaqub Al- urduniy, ana kitabu Al-muwajahatul-kaamilah Ma'a Rasuuli wa Aalihi

Sheikh Said Ayub ni katika maulamaa maarufu Misri ana kitabu Maalimul-fitan Juzuu mbili

Ustadh Idrisa Al Huseiny Al-magharibiy ana kitabu Al-intiqalus-swaabu fiyl Madhihabi wal-mu'utaqadi

Dkt. As'ad Qasimu kutoka Palestina ana kitabu: Haqiqatu Shi'a'ati al ithnaa shariati

Dkt. Muhammad Bayumiy Mahraaniy wa Misri ana kitabu 'Al-imamatu Ahlul-bait (a.s) juzuu tatu na ana vitabu zaidi ya sitini

Sheikh Mu'utasim Sayyid Ahmad kutoka Sudan ana kitabu "Haqiqatu dhai'atu rihilatiy nahawi madhihabi Ahlul-bait

Mwandishi Muhammad Abdul Hafidh kutoka Misri ana kitabu Limadha anaa Jafariy

Dkt. Ahmad Rasimu Annafiysi ana kitabu Atariyqu ilaa madhi-habi Ahlul -bait

Al -Ustadh Muhammad Al-Kathir ana kitabu Asalafiyatu baina Ahlus-Sunna wal -Imamiyah

Sheikh Rashid Rahmani Al-Hindiy ana vitabu vingi kati ya hivyo ni: Limaa Aswibahatu shi'iyan

As-Sayyid Yasin Al-Mayuti Al-Badaraniy kutoka Syria ana kitabu Yaa laita qaumiy Ya'alamuuna

Al Ustadh Abdul-mu'umin Muhammad Al Hasany kutoka Sudani ana kitabu Binuri Faatimata ihtadaitu

Al Ustadh Mutawakil Muhammad Ali kutoka Sudan ana kitabu Wadakhaltu Tashayu'an Sujadan

As-Sayyid Husein Al-Rajaah kutoka Syria ana kitabu Difau min Wahyi Shariati Dhidu dairati Sunnati wa Shi'ati

"Hakika sisi tuliposikia uongofu tuliuamini, atakayemwamini Mola wake basi hataogopa upungufu wala vitisho."1

1. Suratul- Jinn: 13

# Itikadi ya Shi'a Kwa Ufupi

Itikadi ya Shi'a ni itikadi ya Ki-Islamu aliyokuja nayo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kwa misingi yake ifuatayo:-

## Tauhid (Upweke)

Shi'a wanamwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola mmoja na wanamkanusha Mungu asiyekuwa yeye na anayemwabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mshirikina, na wao wanamtakasa Mwenyezi Mungu kutokana na kila aibu na upungufu, na wanathibitisha sifa ambazo zinalingana na Utukufu wake, hafanani na chochote, ana majina mazuri, ame epukana na dhulma na upuuzi, mwadilifu, mwenye hekima "Sema, Mwenyezi Mungu ni mmoja, Mwenyezi Mungu ndio mwenye kukusudiwa, hakuzaa wala kuzaliwa na wala hana anayelingana naye."1

## Nubuwwah (Utume)

Shi'a waanamini Mitume wote ambao wametumwa na Mwenyezi Mungu na katika itikadi yao ni kwamba atakaye mkanusha mmoja wao basi ni kafiri, na wa mwisho wao na mbora wao ni Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w). Mitume ni ma'asum (wamehifadhiwa) kutokana na madhambi madogo na makubwa, hifadhi ya jumla "Hawamuasi Mwenyezi Mungu na wanafanya waliyoamrishwa" na ni wajibu kuwatii "aliyokuleteeni Mtume yachukueni na aliyokukatazeni yaacheni"2 na wao wanawatukuza Mitume na wanawaepusha kutokana na upungufu, na kutokana na waliyonasibishiwa nayo kama vile kauli

inayosema kwamba Mtume alikuwa anazunguka kwa wake zake kumi na mmoja kwa muda wa saa moja[3] na kwamba yeye (s.a.w.w) alikuwa anamlaani asiyestahili kulaaniwa[4] na kwamba alikuwa anawawatesa baadhi ya watu[5] na kwamba alikuwa anasahau katika sala yake[6], na kwamba alikuwa anajisaidia haja ndogo katika Vichochoro.[7]

## Al -Miad (Siku Ya Mwisho)

Shi'a wanaamini kwamba kuna siku Mwenyezi Mungu atawakusanya viumbe wote na kuwalipa kutokana na vitendo vyao hivyo, waumini wataenda peponi na makafiri wataenda motoni, na wanaamini kaburi, pepo, Mizani, swiratwa......

## Al-Adl (Uadilifu)

Uadilifu ni sifa miongoni mwa sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, Shi'a wanaamini na wanaitakidi kwamba vitendo vyote vya Mwenyezi Mungu ni viadilifu na vyenye hekima na kwamba Yeye hamdhulumu yeyote hata kwa kiasi cha punje ndogo kabisa, kinyume na rai ya Ash'ariah ambao wasema kwamba inawezekana kwa Mwenyezi Mungu kuwa adhibu waumini...

## Al-Imamah (Uimamu)

Shi'a wanasema kwamba Mtume (s.a.w.w) kabla ya kufariki alimteua Ali (a.s) kuwa khalifa wa Waislam[8]"na anafuatiwa na maimamu kumi na moja katika kizazi chake, wataongoza umma baada ya kuondoka Mtume (s.a.w.w) lakini yalitokea mapinduzi ambayo yametajwa katika Qur'an. "Hakuwa Muhammad isipokuwa ni Mtume, walishapita kabla yake Mitume, je, akifa au akiuliwa mtageuka nyuma kwa visigino vyenu? Na atayegeuka kwa visigino vyake, hatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa chochote Mwenyezi Mungu atawalipa wenye kushukuru."[9]

Na maimamu aliowateua Mtume (s.a.w.w) baada yake ni maimamu kumi na mbili. Aliwaashiria katika Sahihi Muslim: "Dini haitaacha kuwa yenye kusimama hadi Qiyama kifike au watakuwa kwenu makhalifa kumi na mbili wote kutoka katika Makuraishi."[10]

Na kutoka kwa Jabir bin Samra amesema, "nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), akisema Uislam hautaacha kuwa na nguvu hadi watimie makhalifa kumi na mbili.
Kisha akasema neno sikulifahamu nikamuuliza, baba yangu amesemaje? Akasema, amesema wote ni katika makuraishi."[11]

Na maimamu wa Ahlul- Bait ni: -

1 Imam Ali bin Abi Talib (a.s)-Amirul-mu'uminina

2 " Hasan Bin Ali -Al-Mujtaba (a.s)

3 " Husen bin Ali Shahid (a.s)

4 " Ali bin Huseini-Zainul-Abidin (a.s)

5 " Muhammadi bin Ali-Al-Baqir (a.s)

6 " Ja'fari bin Muhammadi-As-Swadiq (a.s)

7 " Musa bin Ja'far-Al-Kadhim (a.s)

8 " Ali bin Musa-Ar-Ridhaa (a.s)

9 " Muhammadi bin Ali Al-Jawad (a.s)

10 " Ali bin Muhammadi-Al-Haadiy (a.s)

11 " Hasani bin Ali-Al-Askary (a.s)

12 " Al-Hujjatu bin Hasani-Al-Mahdi (a.s)

1. Suratul- Ikhlas
2. Suratu- Hashr :7
3. Sahih Bukhary kitabul-ghusul babu idha jama'a thuma aada waman Daara alaa nisaihi fiy ghusuli wahidi
4. Sahih Muslim kitabul-biri waswilati wal-aadaabu
5. Sahihi Bukhari kitabu twib babu daawai bi abuwali-Ibil
6. Fatuhul-bar J : 1 uk-328
7. Sahihi bukhary kitabul-adab babu maayajuzu min dhikiri naasi Sahihi kitabu masj wadhiu swalat babu sahau Fiy swalati wasujudi lahu.49 Na kuna dalili zilizo wazi juu hilo katika vitabu vya Ahlus sunna, kwa ziada kuhusu maudhui haya rejea kitabu cha Al- ghadiri,cha Sheikh Al-amin, Ihqaqul-haqi cha Tasatary na kitabu chetu warakibtu safinati tunajibu baadhi shubuhati zilizotolewa kama vile,shura,uimamu na Abubakari kuswalisha watu
8. Na kuna dalili zilizo wazi juu hilo katika vitabu vya Ahlus sunna, kwa ziada kuhusu maudhui haya rejea kitabu cha Al-ghadiri,cha Sheikh Al-amin, Ihqaqul-haqi cha Tasatary na kitabu chetu warakibtu safinati tunajibu baadhi shubuhati zilizotolewa kama vile,shura,uimamu na Abubakari kuswalisha watu
9. Suratul-Imraan: 144
10. Kitabul-Imaara, babu Anaasu tabaul-quraish Walkhilafatu fiy quraish
11. Kitabul-Imaara, babu Anaasu tabaul-quraish Walkhilafatu fiy quraish

# Utaratibu Wa Ahlul-Bait (a.s)

Utaratibu wa Ahlul-Bait (a.s) umesimama juu ya kushikamana na Kitabu na Sunna na kuepukana kutoka na kufuata qiyasi na rai ....... Imamu Ali (a.s) alishaandika Sunna Wakati wa Mtume (s.a.w.w) na kitabu chake kimejulikana kwa jina "Aswahifah" na Maimamu wa Ahlul-Bait wanaachiana kitabu hicho na wamekitegemea kwa mapokezi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w). Na hizi ni baadhi ya kauli za maimamu ili

tujue mshikamano wa manhaji yao iliyo madhubuti.

Aliulizwa Imamu Swadiq (a.s) kwa kitu gani Imamu anatoa fatwa? Akasema; kwa kitabu, muulizaji akasema kama hakipo katika kitabu. Imamu akasema, kwa sunna. Muulizaji akasema kama halipo katika sunna? Imamu akasema: hakuna kitu isipokuwa kinapatikana ndani ya kitabu (Qur'an) na sunna. Amesema Imamu Ja'far As-swadiq (a.s), "Hadith yangu ni Hadith ya baba yangu, na Hadith ya baba yangu ni Hadith ya babu yangu na Hadith ya babu yangu ni Hadith ya baba yake, na Hadith ya Ali bin Abi Talib ni Hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na Hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.[1]

"Fuata watu ambao wanasema katika kauli yao na Hadith yao, amepokea babu yetu kutoka kwa Jibrili kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

Amesema Imam Baqir (a.s): "kama tungewaeleza kwa maoni yetu na matamanio yetu basi tungekuwa ni katika wenye kuangamia, lakini tunawaeleza Hadith ambazo tumezihifadhi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kama wanavyohifadhi hawa dhahabu na fedha zao." Mtu mmoja alimlaumu Iban Taghlab juu ya mapenzi yake kwa Imamu Baqir, na kupokea kutoka kwake akasema, "vipi unanilaumu kwa kupokea kwangu kwa mtu ambaye sikumuuliza juu ya kitu isipokuwa husema: "Amesema, Mtume wa Mwenyezi Mungu..."

1. Maalimu-shariati cha sub-hi Swalehe uk:52

# Shutuma Kuhusu Imamiya

Hakika walioandika kuhusu Shi’a walikwepa ukweli pale waliporejea vitabu vya wapinzani na wakanukuu kutoka kwao bila ya kuhakiki wala kutazama. Amesema Hamidi Daud Hanafiy: "Anakosea sana anayedai kwamba yeye anaweza kudhibiti juu ya itikadi ya Shi’a Imamia, elimu zao, na adabu zao kwa yale yaliyoandikwa na wapinzani kuhusu wao, vyovyote watavyofikia hawa wapinzani katika elimu na utambuzi, na vyovyote watakavyokuwa na uaminifu wa kie- limu katika kunukuu hoja na kuzifafanua kwa njia safi iliyoepuka na ta'asubu ya upofu, nasema haya nikiwa na uhakika wa usahihi wa ninayoyasema...[1]

Leo hii tunakuta katika maktaba za Ki-Islam vitabu kiasi 5,000 na makala za kushambulia Ahlul-Bait, na kuwakimbiza watu kutoka kwao, wameeneza picha mbaya juu ya Itikadi yao ambapo wameeleza Ushi’a kama wanavyotaka wao, sio kama ulivyo, na kwa kuwa utafiti wetu huu ni hatua tu, katika njia ya kubainisha haki hakuna budi ya kueleza baadhi ya shutuma ili tuziondoe katika kioo safi cha Ki-Islamu.

## Shutuma ya Ghuluu (Kusifu Kupita Kiasi)

Wametuhumiwa wafuasi wa Ahlul-Bait (a.s), kwamba wao wamesema kuwa maimamu ni waungu, na yanayofanana na hayo katika ghuluu. Ukweli ni kwamba kauli hizi ni za baadhi ya makundi ya waliovuka mipaka, lakini yamenasibishwa kwa Shi'a kwa kutokujua au kwa kujifanya kutokujua, na Shi'a kwa kuwafuata maimamu wao (a.s) wamekanusha kauli hizi na wanakufurisha wanaosema hivyo na hizi ni baadhi ya kauli za maimamu wa Ahlul-Bait ambazo zimebainisha msimamo wao kwa ghuluu na maghulaat.

Imam Sadiq (a.s) amemwambia Swalehe bin Sahl: "Ewe Swalehe: Hakika sisi ni waja tumeumbwa tu na Mola, tunamwabudu na tusipomwabudu atatuadhibu.2

Amesema Imam Ridha (a.s): "Mwenyezi Mungu awalaani Maghulaati, ee sio wengine ila ni Wayahud, ee walikuwa ni Manaswara, ee walikuwa ni Majusi, ee walikuwa ni Marjiah, ee walikuwa Haruriyah," akasema, "msikae nao, msiwa-amini, epukaneni nao na Mwenyezi Mungu yuko mbali nao."3

Na amesema Sheikh Al-Mufid mmoja wa maulamaa wa kubwa wa Kishi'a: Maghulat ni katika wanaojidhihirisha na Uislamu, wao ndio wanaomnasibisha Amiril-Mu'uminina na kizazi chao kwenye uungu na Utume na wakamsifu kwa fadhila katika dini na dunia hadi wakaruka mpaka wakatoka katika makusudio na wao ni wapotevu na ni makafiri. Amirul-Mu'uminina aliwahukumu wauliwe na kuchomwa kwa moto, na maimamu walishahukumu kuwa wao ni makafiri na kwamba wametoka katika uislamu."4

Na amesema Mustafa Shakah akitetea Shi'a kwamba wao wanajiepusha mbali na kauli zilizokuja katika ndimi za baadhi ya vikundi, na wanavihesabu kuwa ni katika ukafiri na upotevu."5

Amesema Urufan Abdul Hamid: "Hivyo si vinginevyo isipokuwa ni katika njia ya kuchafua na yenye kufedhehesha kuingiza mafunzo ya Maghulaat katika Mustwalaha wa Kishi'a, na kuanzia hapa ulidhihiri ufisadi wa hukumu za kijeuri ambazo wamezisema baadhi juu ya Shi'a na kwa sura inayopingana na ukweli ambapo wamewazulia. Na katika mfano wa haya amesema Jauladi Zahiyr, Faridi Landar, Ahmed Amin na wengine dhidi ya Shi'a."6

## Qur'an Tukufu

Wamedai baadhi ya waandishi, kuwa Shi'a wanasema kuwa Qur'an imepotoshwa, tuhuma hii ni batili, wameijibu maulamaa na wamepinga riwaya zilizopokewa kuhusu jambo hili, hata maulamaa wa Kisuni wametetea Shi'a.

Amesema Dkt. Muhammada Abdilah Daraaz "Vyovyote iwavyo, hakika Msahafu ni mmoja uliopo katika ulimwengu wa Ki-Islamu, likiwepo kundi la Shi'a, tangu muda wa karne 13, na hapa tumetaja Rai ya Shi'a Imamiya."7

Na amesema Sheikh Muhammad Ghazali: "nimesikia kwa hawa wanaosema katika mihadhara ya

kielimu, kwamba Mashi'a wana Qur'an nyingine inazidi na kupungua hii yetu maarufu, nikamwambia Qur'an hii iko wapi? Na kwa nini binadamu na majini hawajapata nakala kwa muda wote huu mrefu? Uzushi huu ni wa nini? Uongo huu ni wa nini? Dhidi ya watu na wahyi."[8]

Amesema Sheikh Saduuq aliyefariki 381 H – (mwanachuoni wa Hadith wa Kishi'a): "itikadi yetu katika Qur'an ambayo ameiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake Muhammad ni ambayo ipo baina ya Jalada mbili nayo ni ile ile iliyopo katika mikono ya watu na wala sio zaidi ya haya na asemaye kwamba tunasema ni zaidi ya hiyo basi ni muongo;"[9] na amesema Sheikh Mufiyd aliyefariki 413 H, "ama kuhusu upungufu wamesema jamaa katika Shi'a kwamba haikupungua neno, aya wala sura,..... Ama ziada inakataliwa kwa uharibifu wake."[10]

Shi'a wana vitabu vinavyopinga kupotoshwa kwa Qur'an na vinampinga kila anayesema hivyo. Al-Kurki maarufu kwa Muhaqiqu-thaniy ameandika makala katika kupinga kupungua baada ya kupatikana Ijmai juu ya kutokuwa na ziada, na ametunga Agha Barazak Atwahraniy kitabu "Anaqidulatwif fiy nafiy Atahariyf anil-Qur'an-Shariyf."

Ametunga mmoja wa Maulamaa wa Ahlus-sunna kitabu ili kuthibitisha kupotoshwa kwa Qur'an akakiita "Al-furqan" na wakampinga maulamaa wa misri katika wakati wake;[11] na zinap- atikana katika vitabu vya Ahlus-sunna riwaya nyingi zinazoashiria kupotoshwa kwa Qur'an na hasa katika Sahihi Bukhariy na Muslim.[12]

Kutoka kwa Aisha amesema kwamba "ilikuwa katika yaliyoteremshwa katika Qur'an Aya hii): (Ashara radhaati maalumaati yuhramna thuma musakhina bikhamisi maalumaati) na Mtume wa Mwenyezi Mungu amefariki nazo ni katika aya zinazosomwa katika Qur'an.[13]

Kwa ufupi ni kwamba hakika riwaya hizi ama ziwe kwa Shi'a au kwa Sunni ni riwaya za uongo na zinapingwa na Qur'an imehifadhiwa kutokana na kupotoshwa kwa kuhifadhiwa na Mwenyezi Mungu. Amesema Mwenyezi Mungu: "Hakika tumeiteremsha Qur'ani na hakika sisi ni wenye kuihifadhi"[14] Hii ndio rai ya Shi'a, ama msahafu wa Fatmah (a.s), hio sio Qur'an nyingine bali humo kuna riwaya ambazo zinafungamana na mustakabala wa umma wa Ki-Islam........

1. Katika utangulizi wa Hamid Daudi Hanazi katika "Aqaidul-Imamiya cha mudhafar
2. Sharhe Itikaat Saduuq
3. Uyuunu Akhibar Ridhaa cha Saduq
4. Sharhe Itiiqadi Suduuqu
5. Islamu bila madhaahib
6. Dirasaatu fiyl-firaqiwal-aqaidil-slaamiyatu uk 32
7. Madikhalu ilaa-Qur'anil - kariym uk 39 - 40
8. Difau an aqiidati wa shari'ah. na katika waliotetea Shia dhidi ya tuhuma hii ni Sheikh Muhammad Abu Zahra. Sheikh Rahmatullah Al-Hindi, Ust.Muhamad Madani, na Dkt. Mustafa Rafii
9. Risaalatu itiqaadati
10. Awailul-maqaaati -uk. 55
11. Jarida la Risalatu l-islaam toleo la nne makala ya ustadhi Muhammadul- madainiy uk 382-383
12. Rejea sahihi Bukhariy kitabul-hudud babu rajml- habla mina zinaa. Sahihi Muslim babu lau anna liibni Adam wadiyani

laibtaghaa thalithan, na kitabu ridhaa J:4 uk 167,musnad Ahmad J:5 uk-132

13. Sahihi Muslim kitabu ridha'a babu tahriym bikhamsi radhaat

14. Suratul- Hijr:9

# Taqiya

Inawezekana kufahamu kimakosa taqiya ndiko ambako kume sababisha baadhi kuwashambulia Shi'a, hakika Shi'a hawakujificha vitabu vyao vya rejea ambavyo humo wamechukua itikadi yao vime-enea, na wao wamevichapisha na kuvisambaza kwa watu wa madhehebu mbalimbali, taqiya sio udanganyifu, hadaa na unafiki kama wanavyoita baadhi lakini nikuficha itikadi katika baadhi ya nyakati kwa kuzuia adha kwa wengine.

Sheikh Mufiyd ameelezea kuwa; "ni kuficha haki na kustiri itikadi humo na kuwaficha wapinzani na kuacha kuidhihrisha, kwa yale yanayoleta madhara katika dini na Dunia. Na hivyo ni faradhi kama akijua kuwa kuna madhara au akipata dhana yenye nguvu, asipojua kuwa kuna madhara kwa kuidhihirisha haki wala hajapata dhana yenye nguvu juu ya hilo, sio wajibu kufanya taqiya."1

Na taqiya ambayo kwayo wametuhumiwa Shi'a imeruhusiwa katika uislam, anasema Mustafa Rafi: Taqiya ni kitendo cha kisheria katika uislam, kama ambavyo iliruhusiwa katika zama zilizotangulia kwa jamii zote, umma na dini, na dalili ya kuruhusiwa kwake ni kauli ya Mwenyezi Mungu: ni "Waumini wasiwafanye makafiri kuwa ni marafiki badala ya waumini na anayefanya hivyo hana chochote kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa mkiogopa kwao madhara."2 Hii ina maana kuwa inajuzu kuamiliana nao kwa kufanya taqiya ili kujilinda na adha zao.3

Na amesema Razi katika tafsiri ya Aya "***Ila antataqu min hum tuqaatu***." Imepokewa kutoka kwa Hasan kwamba anasema: "Taqiya inajuzu kwa waumini hadi siku ya Qiama, na kauli hii ni bora, kwa sababu kuzuia madhara kwa nafsi ni wajibu kadir iwezekanavyo. Masahaba wamefanya taqiya ambayo wanaifanya Shi'a, huyu ni Ammar bin Yaasir (r.a) alidhihirisha kwa ulimi wake ukafiri; hali moyo wake umetulizana kwa Imani, basi ikateremka kauli yake Mwenyezi Mungu "isipokuwa aliyelazimishwa na moyo wake umetulizana kwa imani;"4 na Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: "kama watarudia basi rudia kusema hivyo kwani Mwenyezi Mungu ameteremsha kwa ajili yako (Aya ya ) Qur'an na amekuamuru urudie kama watarudi kwako.

Wafuasi wa Ahlul-Bait (a.s) na kwa matokeo ya hali ngumu ambazo zilipita kwao walikuwa wanafanya taqiya kama alivyofanya Ammar (r.a) na sheria hii ambayo imeshuka kwa ajili ya Ammar ni sheria kwa Waislam wote ambapo zingatio ni kwa ujumla wa tamko na sio kwa ajili ya sababu mahsusi.

Mustafa Raafiy amesema katika kutetea Shi'a; "Hakika wale ambao wanawalaumu Shi'a Imamiya kwa kufanya taqiya kwa ajili ya kuhifadhi maisha yao na damu zao, wanawatuhumu kwa tuhuma kali kwa

sababu ya kufanya kwao taqiya badala ya kupigana jihadi na kupambana, je, hawa wanaotuhmu hawakutazama nyuma ili waone kwa yakini kwamba taqiya imeruhusiwa na inaendelea tangu kwa Nuhu, Mu'umini wa Al-Firauni, Musa, ambaye alitoka Misri akiwa na hofu akijificha ambapo amesema, "Basi nikakimbia kutoka kwenu nilipowaogopa.."[5]

Na kwa ndugu yake Haruna aliposema (kaumu imenionea na walikaribia kuniuwa"[6] Na kwa Lut aliposema: "Kama ningekuwa na nguvu kwenu au nijifiche katika ngome madhubuti.."[7] hadi kwa mwisho wa Mitume, Mtume Muhammad bin Abdillah (s.a.w.w). Je, yeyote atajaribu kuwatuhumu hawa Mitume? Na wengi wao ni katika Ulul-Azmi kwa kukimbilia kwao kwenye udanganyifu na kuacha jihadi kama wapinzani wanavyowatuhumu Shi'a Imamiya? Mimi sidhani kama binadamu mwenye akili, mwadilifu hataona udhuru wao katika kutumia taqiya bali ataona ni wajibu kwao kufanya taqiya badala ya kuwanasibisha kwa sababu yake kwenye udanganyifu, hila na unafiki.[8]

1. Taswihihul-itiqaad uk:115
2. Suratul Imraan: 23
3. Islaamunaa fiy taufiyq baina sunna wa Shiati uk : 135
4. Suratu Nahl: 106
5. Suratu Shu'araa: 21
6. Suratul - Aaraf: 150
7. Suratu Hud: 80
8. Islaamunaa 133 - 134

# Turbah ya Husein

Ma-Shi'a wanatumia turbah (kipande cha udongo) iliyotengenezwa kwa udongo kusujudia juu yake, na baadhi ya waandishi wamepata fursa ya kushambulia Shi'a, na katika kufafanua jambo hilo tunasema: "Hakika kanuni katika madhehebu ya Ahlul-Bait ni kwamba haijuzu kusujudu isipokuwa kwenye ardhi au kilicho ota ardhini ukiondoa vinavyoliwa na kuvaliwa.

Na baada ya kufa shahidi Imamu Husein imekuwa ni ada kwa Shi'a na kwa maelekezo kutoka kwa maimamu wao kusujudu juu ya Turbah ya Karbala, wao wanasujudu juu ya Turbah na sio kuisujudia, kama wanavyodai wapinzani, kama vile Sunni wanaposujudu juu ya Sujada, wanasujudu juu yake na wala hawaisujudii ...

Na masahaba walikuwa wanasujudu juu ya changarawe na Mtume (s.a.w.w) hakuwakataza.

Anasaai amepokea kutoka kwa Jabiri bin Abdillah amesema "Tulikuwa tunasali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu Adhuhuri basi nilikuwa nachukua changarawe kwa kiganja changu nazipooza kisha ninazihamishia kwenye kiganja kingine, ninaposujudu naziweka mahali ninapoweka paji la uso wangu."[1]

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikuwa anasujudu juu ya mchanga, vile vile juu ya udongo kama ilivyo katika Sahihi Bukhariy."2

Na amesema Mtume (s.a.w.w): "Nimefanyiwa ardhi kuwa ni mahali pa kusujudia na ni tohara."3 Hivyo inajuzu kusujudu juu ya udongo kwa sababu ni sehemu ya ardhi na hakuna tofauti baina ya mtu kusujudu juu ya udongo au kutengeneza Turbah ya kusujudia juu yake kutoka kwayo, huu ni udongo na ule ni udongo na wala haizingatiwi tofauti ya umbo.

Mas'ala ya kusujudu juu ya udongo yanabaki kuwa ni mas'ala ya kifiqihi ambayo Shi'a wametofautiana na madhehebu mengine, kama ambavyo kila moja katika madhehebu manne lina mas'ala mahsusi linalofautiana na mengine, na Shi'a katika mas'ala haya na mengineyo wamefuata yaliyo sahihi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w).

1. Sunanu nasaaiy J: 2 babu Tabriydil - haswaa
2. Sahihi Bukhariy J: 2 kitabul itiqaaf katika kumi la mwisho
3. Sahihil Bukhariy kitabu tayamam

# Al - Badau

Al-badau ni tuhuma miongoni mwa tuhuma ambazo wapinzani wa Shi'a wanaieneza dhidi yao kwa msukumo wa kimadhehebu bila ya kutazama kwa kina katika kusoma hoja ambazo Shi'a wamefahamu kutoka kwayo. Bali wapinzani wa Shi'a wanazidi kuelekeza tuhuma na kuwalaumu kwa sababu yake hadi Al-badau imekuwa ni moja ya tofauti za kimadhehebu ambazo zimetenganisha Shi'a na wasio kuwa wao.1

Badau kwa Shi'a ni kuongezeka umri na riziki na kupungua kwake kutokana na vitendo.2

Wanadai baadhi ya waandishi kwamba badau wanayoisema Shi'a ni kudhihiri kwa Mwenyezi Mungu yaliyokuwa hayafahamiki kwake. Na kauli hii ni batili, Shi'a wako mbali nayo. Lakini badau kwao ni kudhihiri baada ya kufichwa na sio kudhihiri baada ya kufichikana, Mwenyezi Mungu wakati kinadhihiri kitu kwake tayari yeye ana elimu tangu awali ya hili linalodhihiri kwake." Amesema Imam Swadiq (a.s): "Hakika hakidhihiri kitu kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa kitakuwa katika elimu yake kabla ya kudhihiri kwake," na amesema (a.s): "Hakika Mwenyezi Mungu haidhihiri kwake ambako kumetokana na kutokujua."3

Na badau ipo katika itikadi ya Sunni ispokuwa haikufanyiwa utafiti kwao kama ilivyofanyiwa katika Shi'a.

Amepokea Bukhariy kutoka kwa Abu Huraira kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) Amesema: "hakika watu watatu katika Bani Israili wana mbalanga, kiziwi na kipofu ilidhihiri kwa Mwenyezi Mungu

kwamba awape mtihani."[4]

Na kisa ni kirefu katika sahihi Bukhariy na mahala pa ushahidi hapa ni kauli yake (s.a.w.w) (Badaa lillahi) (ilidhihiri kwa Mwenyezi Mungu). Mtume (s.a.w.w) amenasibisha Albadau-ambayo wanaisema Shi'a kwa Mwenyezi Mungu, je, watajibu? Hao wapinzani ambao wanatuhumu Shi'a juu ya itikadi yao hii? Na katika Sahihi Muslim kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anasema: "Anayependa akunjuliwe riziki yake au arefushiwe umri wake basi na auunge udugu wake."

Amesema Nawawiy katika kusherehesha Hadith: Ama kuahirisha mauti humo kuna suala mashuhuri nalo ni kwamba mauti na riziki zimekadiriwa haziongezeki wala hazipungui, inapokuja ajali yao hawacheleweshwi hata saa moja wala hawawahishwi. Na maulamaa wanajibu majibu sahihi juu ya hilo.

Jibu la pili- Ni kwamba kuhusu yanayodhihiri kwa Malaika, katika lauhul-mahfudh na mfano wa hayo, inadhihirika kwao katika lauhul-mahafudh kwamba umri wake ni miaka sitini isipokuwa akiunga udugu wake anazidishiwa arobaini, na Mwenyezi Mungu mtukufu anajua yatakayomtokea kwa ajili ya hiyo, nayo ndiyo maana ya kauli yake (s.a.w.w) "Anafuta anayotaka."

Na anathibitisha humo kulingana na elimu ya Mwenyezi Mungu na ambayo yametanguliwa na kudra yake kwamba hakuna ziada bali ni mustahili. Na kwa yaliyodhihiri kwa viumbe yanatupa picha ya kuongezeka, na ndio kusudio la Hadith.[5]

Haya ambayo ameyataja Nawawiy ndio badau halisi ambayo wanaisema Shi'a, na Aya aliyotolea dalili kwayo, ya kuunga mkono itikadi hii, ndio ile ile wanayoitolea ushahidi Shi'a.

Amesema Dkt. Hamid Daud Hanafiy: "Ilipokuwa badau ni katika sifa za viumbe, kwa sababu kufanya kitu kisha kukifuta inaonyesha fikira inayojitokeza, na kusahihisha baada ya kukosea na kufahamu baada ya kutokujua, hivyo wanafikra wengi wamepuuza akili za Mashi'a kwa kunasibisha badau kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, na Shi'a wako mbali ambapo kilichobainikiwa kwao na kwa Maulamaa wa Kisuni ni kwamba elimu ya Mwenyezi Mungu ni ya zamani imeepukana na mabadiliko na kufikiri ambavyo ni katika sifa za viumbe.[6]

1. Islaamunaa uk: 210
2. Awailul-maqaalati-ya Sheikh Mufiyd
3. Usul-kaafiy J: I uk:148
4. Sahihi Bukhariy kitabul- Ambiyai - Hadith abras wa a'amaa wa aqirasu fiy bani Israil
5. Sahihi Muslim sharhe ya Nawawiy kitabul-biru wa swilatu wa adaabu babu swilatu rahmi wa tahariymi Qatwi'uhu
6. Utangulizi wa "kitabu cha Aqaudul - Imamiyah uk: 25

# Raja'ah

Raja'ah: kwa Shi'a ina maana kwamba Mwenyezi Mungu atawarejesha katika siku za mwisho wa Dunia watu miongoni mwa wafu katika wale waliobobea katika imani na wale waliobobea katika ukafiri, Mwenyezi Mungu atalipiza kisasi hawa kwa wale.

Na itikadi hii sio muhimu sana katika madhehebu ya Shi'a na haina uzito kwa Shi'a ni kama vile imani juu ya Dajali na mambo mengine, amesema Kaashiful-Ghitrwaa.

Mmoja wa maulamaa wakubwa wa Kishi'a - kuamini raja'ah katika madhehebu la Shi'a sio lazima na wala kutoiamini kwake hakudhuru na wala Ushi'a haukuambatanishwa nayo kwa kuwepo au kutokuwepo kwake, nayo si kingine bali ni kama vile baadhi ya habari za ghaibu na matukio yajayo, masharti ya Qiyama mfano wa kushuka Isa kutoka mbinguni, kudhihiri Dajali, kutokea Sufiyani n.k. miongoni mwa mambo yaliyoenea kwa Waislamu nayo sio chochote katika Uislamu, kutoyaamini kwake sio kutoka katika Uislamu na wala kuyaamini kwake sio kuingia katika Uislamu, ndivyo ilivyo raja'ah."[1]

Na raja'ah ni mahala pa ikhitilafu baina ya maulamaa wa Kishi'a, kati yao wameithibitisha na kati yao kuna wanaoikanusha ...hakika raja'ah baadhi wameikuza na wakaihesabu kuwa ni katika misingi ya Ushi'a kwa uongo na uzushi.

Na raja'ah sio kwamba haiwezekani, baada ya kuwa ilishatokea katika kaumu zilizotangulia, katika Qur'an kuna sehemu nyingi kuhusu kurejea baadhi ya wafu katika uhai, mfano: "Uzair" ambaye Mwenyezi Mungu alimfisha miaka mia moja kisha akamfufua."[2]

Na wafuasi wa Musa waliotaka kumuona Mwenyezi Mungu, basi wakapatwa na mauti: Amesema Mwenyezi Mungu "Kisha tukawafufueni baada ya kufa kwenu huenda mtashukuru."[3]

Suyutwiy amesema kuhusu raja'ah lakini kwa maana inayotofautiana na waliyoisema Shi'a yeye amedai uwezekano wa kumuona Mtume (s.a.w.w) ukiwa macho, na ametunga kitabu juu ya hilo nacho ni "Imkaniyatu ru'uyatii Nabiyyi wal-malakati fiy yaqadhah (uwezekano wa kumuona Mtume na Malaika ukiwa macho). Na amedai kumuona kwake Mtume (s.a.w.w) zaidi ya mara Sabini akiwa macho.

Na amesema Aswabaan Ashaafiy kuhusu kurejea Mtume (s.a.w.w) baada ya kuzungumza juu ya njia za Isa kujua hukumu za Ki-Islamu baada ya kudhihiri kwake akasema: "Na kati ya njia hizo ni kwamba Isa atakaposhuka atakutana na Mtume (s.a.w.w) hivyo hakuna kizuizi cha kuchukua kutoka kwake anayoyahitaji kutoka kwake miongoni mwa hukumu za Kisheria."[4]
Amesema Dkt. Ali Abdul-wahlid Wafiy akitetea Shi'a: "Vyovyote iwavyo hakika kuitakidi kwa moja ya raja'ah mbili au zote mbili hakumtoi mwenye kuitakidi kwenye Uislamu."[5]

Baada ya safari hii fupi juu ya mawimbi ya kuvumbua zana iliyofichikana imetubainikia umuhimu wa

madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s) baina ya madhehebu zingine, umadhubuti wa misingi yake na ubora wa kujiunga nayo.

Pamoja na kwamba wapinzani wanaeneza uongo wa kuzua juu ya madhehebu ya Shi'a isipokuwa waadilifu katika maulamaa wa Ahlus-sunna wameandika wazi kuhusu kundi hili, baadhi yao wameyahesabu kuwa ni madhehbu ya tano na wakaifanya kuwa ni kioo cha mwisho cha Ki-Islamu kilicho safi na hizi ni baadhi ya kauli zao:

Imamul-Akbar Sheikhul - Azhari Mahmud Shaltut amesema: "Hakika madhehbu ya Ja'fariyah maarufu kama madhehebu ya Shi'atul-Imamiya; ni madhehebu yanayojuzu kufanya ibada ya Kisheria kwayo, kama madhehebu mengine ya Sunni."[6]

Sheikhul - Azhari Dkt. Muhammad Muhammad Al-Fahaam amesema: "Sheikh Shaltut mimi nilikuwa kati ya wanaovutiwa naye kwa tabia yake, elimu yake, upana wa fahamu yake na uwezo wake wa lugha ya Kiarabu, tafsiri ya Qur'an na kusomesha kwake Usulul-fiqihi, na ameshatoa fatwa juu ya hilo, yaani kujuzu kufanya ibada kwa mujibu wa madhehebu ya Shi'atul-Imamiyah - hapana shaka ametoa fatwa ambayo imejengeka juu ya msingi katika itikadi yangu. "[7]
Mwenyezi Mungu amrehemu Sheikh Shaltuti ambaye ametambua maana hii tukufu hivyo ukadumu katika fatwa yake ushujaa, kwa kujuzu kufanya amali kwa mujibu wa madhehbu ya Shi'a Imamiyah."[8]

Sheikh Muhammad al-Ghazaaliy amesema: Naitakidi kwamba fatwa ya Ustadh mkubwa Sheikh Mahmud Shaltut, imepiga hatua kubwa katika njia hii na mwanzo wa juhudi za mwenye ikhilasi miongoni mwa watu wenye mamlaka na wenye elimu wote, na ni ukanusho wa ambayo wanayatarajia makafiri wakimagharibi miongoni mwa chuki ambayo itauteketeza umma kabla ya kuungana na safu zake chini ya bendera moja ......fatwa hii kwa mtazamo wangu ni mwanzo wa njia na mwanzo wa vitendo.

Hakika Shi'a wanaamini ujumbe wa Muhammad na wanaona utukufu wa Ali upo katika kushikamana kwake na Sunna zake na wao ni kama Waislamu wengine.

Hawamuoni binadamu katika waliotangulia na katika wajao, mtukufu zaidi kuliko As-swadiqul-amini."[9]

Abdul-Rahmani Annajaar - mkurugenzi wa msikiti wa Cairo - amesema: "Fatwa ya Sheikh Shaltut tunatoa fatwa kwayo hivi sasa tunapoulizwa bila ya kujifunga na madhehbu manne, na Sheikh Shaltut ni Imam mujitahidi, rai yake inapatia ukweli halisi kwa nini tutosheke na fikra zetu na fatwa zetu juu ya madhehbu fulani tu, hali ya kuwa wote ni wenye kujitahidi."[10]

Dkt. Mustafa Raafiy amesema:
"Hayo madhehbu mawili (amekusudia Imamiyah na Zaidia) ya Ki-Islamu ambayo yanakutana pamoja na madhehbu ya Ahlus-sunna na inasihi kufanya ibada kulingana na hukumu zao; na sioni ambayo yanazuia kuitakidi madhehebu ya Ja'fariyah sambamba na madhehebu manne."[11]

Hasan al-Banaa amesema:

Tambueni kwamba Sunni na Shi'a ni Waislamu; linawakusanya neno la "Laa Ilaaha Illa-llaahu wa Anna Muhammadan Rasulu llaahi" na huu ni msingi wa itikadi, na Sunni na Shi'a hapo wako sawa na hapo ndipo wanapokutanika, ama tofauti baina yao ni katika mambo ambayo kuna uwezekano wa kukurubiana baina yao.12

Ustadh Ahmad Beka Al-Masriy, Ustadh Shaltuti na Abu Zahra, amesema, "Shi'atul-imamiyah ni waislamu, wanamwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Qur'ani na yote ambayo alikuja nayo Muhammad (s.a.w.w), na katika Shi'a Imamiyah, zamani na hivi sasa kuna mafaqihi wakubwa sana na maulamaa katika kila fani na wao wanafikra za kina, wapana wa maarifa na utunzi wao unahesabiwa kwa mamia ya maelfu na nimeshasoma mwingi miongoni mwao."13

Sheikhul-Azhar Sayid Muhammad Twantawiy amesema: "Hakika waislamu Sunni na Shi'a wanamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kwamba tofauti za maoni hazipunguzi daraja ya imani za watu."14

Ustadh Mahamud As-Sartwawiy - mkuu wa kitivo cha sheria katika Chuo kikuu cha Jordan na mmoja kati ya watoa fatwa wakuu anasema:

"Hakika mimi nasema ambayo wanayasema: Shi'a Imamiyah ni ndugu zetu katika dini, wanao kwetu haki ya udugu na tunao kwao mfano wa waliyonayo kwetu, yanayopatikana baina yetu na wao miongoni mwa tofauti za maoni hakika ni katika matawi."15

Ustadh Abdul-Fataha AbdulMaqsd anasema:
"Hakika katika itikadi yangu ni kwamba Shi'a wao ni picha ya uislamu sahihi na ni kioo safi na anayetaka kutazama Uislam ni juu yake atazame kupitia itikadi ya Shi'a na kupitia katika vitendo vyao, na historia ni shahidi bora juu ya ambayo wanayafanya Shi'a miongoni mwa huduma kubwa katika uwanja wa kutetea itikadi ya Ki-Islamu.
Na hakika maulamaa wa Kishi'a watukufu ndio ambao wameshika nafasi kubwa ambayo hajaishika yeyote asiyekuwa wao katika nyanja mbali mbali, wamepigana, wamepambana na wamejitoa muhanga kwa ajili ya kuunyanyua Uislamu na kueneza mafunzo yake matukufu, kuwaelimisha watu na kuwaelekeza kwenye Qur'an."16

1. AswiluShiatu wa usuluha uk. 68
2. Suratul- Baqarah: 259
3. Suratul- Baqarah: 56
4. Is'afu-raghibiyna bihaamishi nurul-abswar 161
5. Baina Shiati wa Ahlus-sunnah uk. 57
6. Islamunaa cha Raafiy uk. 59 na ilitangazwa katika jarida la Risaatul-islamu linalochapishwa Misri
7. Fiy sabil-wahdatil - islaamiyah cha Ridhawiy uk
8. Islamuna:59
9. Difaain anil aqiida Uk. 257
10. Fiy sabil wahdahti Islaamiyati cha Murtadha Ridhwi uk:
11. Islaamuna a uk:32 59

12. Dhikriyaatu laa mudhakaraatu cha omar Tilmisaaniy uk: 249, jarida la Al- alam toleo NO: 519 uk : 40
13. Tarekh tashiriul Islam
14. Majalatu thaqalain toleo la pili mwaka wa kwanza - 1413H uk: 252 na 253.
15. Majalatu thaqalain toleo la pili mwaka wa kwanza - 1413H uk: 90
16. Fiy sabilil-wahdatil - islaamyat

# Mwisho

Ni bora kwa waislamu waadilifu kuacha ambayo wameyaandika wapinzani wa Shi'a dhidi yao na waanze wenyewe kwa akili zao utafiti juu ya ukweli. Vitabu vya Shi'a vimeenea kila sehemu na kuna uwezekano wa kuwasiliana na taasisi zao na maulamaa wao.

Si dai katika utafiti huu kwamba mimi nimefikisha Ushi'a wote kwa ukamilifu wake kwa wasomaji, utafiti ni mpana katika jambo hili na muhtasari huu hauwezi ukaubeba wote.

Na ifuatayo ni baadhi ya orodha ya vitabu tunaiweka mbele ya watafiti kwa anayetaka ziada ya utafiti katika maudhui haya:-

Vitabu vya maulamaa na wasomi wa Kisunni ambao uliwaongoza utafiti wa kielimu na tahakiki kwenye ukweli wa madhehebu ya Ahlul-Baiti (a.s) tumetaja baadhi ya vitabu hivyo katika kurasa zilizotangulia:-

Al- Muraa jaatu - cha Sayyid Sharaf Diyni Al-Amiliy.

Al-Ghadiyr - cha Sheikh Al-Aminiy kina juzuu kumi na moja.

Maalimul-Madrasatain - cha Sayyid Murtadha Al-Askariy.

Al-Imamus-Swadiq (a.s) wal-madhaahibil- aruba'a cha Sheikh Asad Haydar.

Layaaliy bishawaari - Munadharatu wal- hiwar cha Sayyid Muhammad Al- Musawi Shirazi.

Aslu Shi'a wa usuuliha - cha Sheikh Muhammad Husein Kashiful Ghitwaa.

Annasu wal- ijtihaadu - cha Sayyid Sharafu Diyni Al- Amiliy.

Nadhariyatu Al-Khalifataini na Ighitiyali Khalifata Abiy Bakar bisumm" vya Sheikh Najaaha Atwaaiy.

Difau an wahyi as-shariati - cha Sayyid Husein Ar-Rajaa.

Na mwisho wa wito wetu ni kwamba, shukrani zote ni za Mola wa walimwengu na sala na amani zimwendee Muhammad na Ali zake wema watukufu.

**Source URL:** https://www.al-islam.org/sw/mbingu-imenikirimu#comment-0

**Links**

[1] https://www.al-islam.org/sw/organization/al-itrah-foundation

[2] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/43497

[3] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/43497

[4] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/43497